german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by:

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

World Vision



# UKUAJI UPYA WA MITI NA MIMEA KWA USIMAMIZ WA MKULIMA (FMNR)

Mwongozo wa warsha kwa Wakufunzi

2024

# Shukurani

Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR) unaangazia changamoto za kimataifa kwa ulimwengu wetu wa sasa. Kupitia kwa FMNR, watu ambao wanaathiriwa kutokana na uharibifu wa ardhi na mabadiliko ya tabianchi wanawezeshwa kurejesha afya ya mfumo wa ikolojia. Kwa hivyo, huu ni mwelekeo ambao unachangia katika kuboresha maisha ya mamilioni ya watoto na jumuiya zao ulimwenguni kote. Kutokana na mchango huu muhimu wa kimataifa, ni suala faafu kwamba mwongozo huu wa warsha ya FMNR umeandaliwa kupitia kwa juhudi za washikadau mbalimbali, ambao World Vision Germany inawashukuru kwa dhati.

Tunashukuru Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Muungano wa Ujerumani (BMZ) kwa kulenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kurejesha mifumo ya ikolojia na kuhifadhi viumbe anuwai. Msimamo wa kisiasa pamoja na wa kifedha na mgao unaoambatana ni muhimu kwa uanzishaji unaofaa na urudufu wa juhudi za FMNRmazingira. Kwa kweli ni fedha kama hizi kutoka kwa BMZ ndizo zimesambazwa kwetu kupitia kwa GIZ, na tunashukuru sana kuwa na ushirikiano wao katika kusambaza FMNR katika kiwango cha kimataifa. Kwa njia mahususi, ni kupitia ushirikiano maalum na mpango wa GIZ wa Forest4Future chini ya Mradi wa Upanuzi wa FMNR nchini Ethiopia na Kenya, ambapo Mwongozo huu wa Warsha ya FMNR umetengenezwa.

Katika World Vision Germany, tunatoa shukurani za dhati kwa Flavia Marà, kwa uratibu mzuri wa jumla, usimamizi wa kiufundi pamoja na michango ya kimaandishi katika hatua zote za maandalizi ya mwongozo huu. Shukurani za pekee
kwa Simon Wittich kwa jukumu muhimu katika usanifu wa dhana ya mafunzo na kuanzisha maandalizi ya mwongozo huu wa warsha. Shukurani pia kwa Liyanda Seither, kwa uratibu wake katika mradi uliotajwa awali, pamoja na kuelekeza mchakato na kusaidia katika kuhariri Dhana na Mwongozo wa Warsha ya FMNR.

Ndani ya Ushirikiano wa World Vision, tunatoa shukurani tele kwa World Vision Kenya na World Vision Ethiopia kwa kushiriki kwa hiari utaalamu wao wa kina katika kupanga FMNR, na kuchangia kuboresha mwongozo huu. Shukurani za pekee kwa Adisu Abebe na Emily Ouko kutoka World Vision Ethiopia na World Vision Kenya mtawalia, ambao walisimamia Mradi wa Upanuzi wa FMNR. Katika wajibu wao, waliongoza michango ya kiufundi na inayohusu maudhui ya ofisi husika na vikundi vya Wataalamu, ambao pia tunawashukuru. Isitoshe, ni muhimu kutambua kuwa waliwezesha majaribio ya Dhana ya Warsha ya FMNR, ambayo ndiyo msingi wa mwongozo huu, katika mafunzo mbalimbali ya FMNR. Jambo hili halingewezekana bila ushirikiano na mipango husika ya FMNR katika nchi hizi mbili. Shukurani tele kwa mipango inayohusika ikiwa ni pamoja na Mpango wa Kurejesha Miti Afrika uliofadhiliwa na Muungano wa Ulaya, Upanuzi wa Mradi wa Ukuaji Upya wa Miti na Mimea wa Bonde la Kati Unaosimamiwa na Wakulima uliofadhiliwa na DFAT, Mradi wa Ukuaji Upya wa Miti na Mimea wa Humbo unaosimamiwa na Jumuiya uliofadhiliwa na Benki ya Dunia, Urejesho wa Afrika uliofadhiliwa na Climate Asset Management na Usimamizi Jumuishi wa Mali Asili kwa Uthabiti katika Ardhi za Maeneo Kame (IMARA) uliofadhiliwa na SIDA.

Tunatoa shukurani za kipekee kwa World Vision Australia. Mwongozo huu wa Warsha za FMNR umechota, umerejelea, na unalenga kuongezea mkusanyiko mkubwa wa matini za maarifa ya FMNR ambazo zimeandaliwa kupitia kwa mipango na ujuzi World Vision Australia kuhusu FMNR. Tunashukuru kwa mwongozo wa kiufundi na msaada uliotolewa na Alice Muller.

Mwisho, tunatoa shukurani za dhati kwa wanaoshabikia FMNR, wanajumuiya, na watoaji wa mafunzo ya FMNR ambao wanazidi kutetea upanuzi wa FMNR kama mwelekeo wa kurejesha na kuhifadhi afya ya mifumo ya ikolojia. Nyinyi ndio mnatoa motisha ya kuandaa mwongozo huu wa warsha, ambao hatimaye unalenga kueneza ujuzi wenu kwa mtandao mpana zaidi wa washikadau wa FMNR, watoaji mafunzo wa siku zijazo na wataalamu. Asanteni kwa kuhamasisha na kuwezesha ukuaji wa mbinu za FMNR katika jumuiya ya kimataifa.

*Martin van de Locht*

**Martin van de Locht,**
**Mkuu wa Mipango ya Kimataifa,**
**World Vision Germany.**

**Waandishi:**

- Flavia Marà, Mshauri wa Kiufundi Utunzaji wa Tabianchi na Mazingira, World Vision Germany
- Adisu Abebe, Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi & Mazingira, World Vision Ethiopia
- Emily Ouko, Meneja – Mradi wa Upanuzi wa GIZ FMNR, World Vision Kenya

**Wahariri/Wakaguzi:**

- Alemayehu Markos, Meneja wa Mradi wa FMNR Mobement Catalyst, World Vision Ethiopia
- Workneh Edesa Huriso, Mratibu wa Miradi ya Mabadiliko ya Tabia nchi na Mazingira, World Vision Ethiopia
- Lavenda Odere, Mratibu wa Usimamizi wa Mali Asili, World Vision Kenya
- Liyanda Seither, Mratibu Mkuu Afrika / Naibu Kiongozi wa Kikundi, World Vision Germany

**Mwongozo wa ziada wa kiufundi:**

- Alice Muller, Mshauri Mkuu wa Ufuatiliaji na Tathmini (FMNR Scale-Up), World Vision Australia
- Yukiko Yamada Morovic, Mkurugenzi wa Kiufundi, Uendelevu wa Kimazingira na Mikakati ya Tabianchi (ESCA), World Vision International

Mhariri wa nakala: Katie Fike

**Usanifu:**

- Daniel Ron Berro, Msanifu wa Michoro, Huduma za Ubunifu, World Vision International Global Ofisi ya Center Manila

World Vision Deutschland e. V.
Am Zollstock 2-4 • 61381 Friedrichsdorf
phone: +49 6172 763-0
info@worldvision.de

Berlin office
Luisentraße 41 • 10117 Berlin

worldvision.de

# Dibaji

Tuna furaha kutanguliza Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR): Mwongozo wa warsha kwa Wakufunzi. FMNR ni mwelekeo ambao unaweza kusaidia katika Urejesho wa ukamilifu wa kiikolojia licha ya uchangamano wa uharibifu wa ardhi. Mbinu hii, kwa kuzingatia ujuzi wa kitamaduni na hatua za mashinani, inalenga kuwawezesha wakulima na Wataalamu kuhuisha mifumo ya ikolojia na kurejesha ardhi iliyoharibiwa kwa kutumia mbinu sahili zenye ufanisi. Mwongozo huu unatoa maelekezo ya kina kwa wawezeshaji, kwa kuwapa ufahamu, stadi, na nyenzo zinazohitajika ili kutekeleza mipango ya FMNR kwa ufanisi. Mwongozo huu ni thabiti kiufundi, na unasheheni sifa ya ushirikiano, ujumuishaji, na uwezeshaji. Unaakisi ufahamu wa pamoja wa wakulima, Wataalamu, na watafiti ambao wameungana kutimiza ndoto wanayoshiriki.



**Yukiko Yamada Morovic,**
**Mkurugenzi wa Kiufundi, Uendelevu wa kimazingira na Mikakati ya Tabianchi (ESCA),**
**World Vision International**



# Yaliyomo

**Shukurani.** . . . . . . . . . . . . **i**
**Dibaji** . . . . . . . . . . . . **iii**
**Yaliyomo** . . . . . . . . . . . **v**
**Orodha ya majedwali na michoro** . . . . . . . . **vi**

1. Utangulizi . . . . . . . . . . . . **09**
2. Azma na walengwa wa mwongozo . . . . . . . **11**
    2.1 Mwongozo huu unalenga nani? . . . . . . . **11**
    2.2 Malengo ya mwongozo huu na warsha . . . . . . **12**
3. Kanuni za ufunzaji za warsha hii . . . . . . . . **13**
4. Masuala ya msingi ya warsha ya FMNR . . . . . . . **15**
    4.1 Ukubwa na muundo wa kikundi . . . . . . . **15**
    4.2 Mahali pa Warsha . . . . . . . . . **16**
    4.3 Ratiba ya warsha . . . . . . . . . **17**
5. Vitengo vya ujifunzaji na masomo. . . . . . . . **19**
    Kitengo 1 cha ujifunzaji: Ufunguzi wa warsha . . . . . **19**
        Somo la 1.1: Makaribisho na utangulizi . . . . . . **20**
        Somo la 1.2: Kanuni na sheria za ufunzaji za warsha hii . . . **21**
        Somo la 1.3: Maudhui ya warsha na malengo ya somo . . . **22**
        Somo la 1.4: Tathmini ya kabla ya warsha . . . . . . **23**
    Kitengo 2 cha ujifunzaji: Uharibifu wa kimazingira, ukataji miti
Na usimamizi wa mali asili ... . . . . . . . . **24**
        Somo la 2.1: Michoro ya uhusiano ya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili (Zoezi la tafakari shirikishi katika kikundi) . . . . . . **25**
        Somo la 2.2: Masuala ya msingi ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili . . . . **32**
        Somo la 2.3: Utangulizi kwa Urejesho wa Misitu na Mandhari (FLR) iliyo katika jamii **35** . . . . . . . . . . .
    Kitengo 3 cha ujifunzaji: Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR) . . . . . . . . . . **37**
        Somo la 3.1: Utangulizi wa FMNR . . . . . . . **38**
        Somo la 3.2: FMNR kama mbinu ya kiufundi . . . . . **42**
        Somo la 3.3: FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii . .. **45**
        Somo la 3.4: Upeo wa kutumia FMNR. . . . . .. . **48**
    Kitengo 4 cha ujifunzaji: Kufunga warsha . . . . . . **51**
        Somo la 3.4: Upeo wa kutumia FMNR. . . . . . . **51**

**Marejeleo** . . . . . . . . . . . . **56**
**Nyongeza** . . . . . . . . . . . . **57**
**Kiambatisho** . . . . . . . . . . . **59**

# Orodha ya majedwali na michoro

## Majedwali

Jedwali 1 Kanuni za ufunzaji wa watu wazima na athari zake kwa mafunzo . 13
Jedwali 2 Kielelezo cha ratiba ya warsha . . . . . . . 17
Jedwali 3 Somo la 1.1 Muhtasari . . . . . . . 20
Jedwali 4 Somo la 1.2 Muhtasari . . . . . . . 21
Jedwali 5 Somo la 1.3 Muhtasari . . . . . . . 22
Jedwali 6 Somo la 1.4 Muhtasari . . . . . . . 23
Jedwali 7 Somo la 2.1 Muhtasari . . . . . . . 29
Jedwali 8 Somo la 2.2 Muhtasari . . . . . . . 34
Jedwali 9 Somo la 2.3 Muhtasari . . . . . . . 36
Jedwali 10 Somo la 3.1 Muhtasari . . . . . . . 40
Jedwali 11 Somo la 3.2 Muhtasari . . . . . . . 44
Jedwali 12 Somo la 3.3 Muhtasari . . . . . . . 47
Jedwali 13 Somo la 3.4 Muhtasari . . . . . . . 50
Jedwali 14 Somo la 4.1 Muhtasari . . . . . . . 51

## Michoro

Mchoro 1 Kitengo 1 cha ujifunzaji: Ufunguzi wa warsha . . . . . . . 19
Mchoro 2 Kitengo 2 cha ujifunzaji: Uharibifu wa kimazingira,
ukataji miti na usimamizi wa mali asili . . . . . . . . 24
Mchoro 3 Kitengo 3 cha ujifunzaji: Urejesho wa Kiasili kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR). 37
Mchoro 4 vipengele vya utendaji wa kiufundi wa FMNR. . . . . . . 42
Mchoro 5 Vipengele vya kimsingi vya FMNR, ikiwemo mbinu nne (nusu duara ya juu)
Na vipengele vitatu vya mchakato (nusu duara ya chini . . . . . . 45
Mchoro 6 Kitengo 4 cha ujifunzaji: Kufunga warsha . . . . . 51

# Orodha ya vifupisho

| | |
|---|---|
| **CGIAR** | Consultative Group for International Agricultural Research |
| **CIFOR** | Center for International Forestry Research |
| **FAO** | Food and Agriculture Organization (of the United Nations) |
| **FLR** | Forest and landscape restoration |
| **FMNR** | Famer Managed Natural Regeneration |
| **GEF** | Global Environmental Facility |
| **IPCC** | Intergovernmental Panel on Climate Change |
| **IUCN** | International Union for Conservation of Nature |
| **NRM** | Natural resource management |
| **UNEP** | United Nations Environment Programme |



# Orodha ya istilahi

**Utafiti tendaji**: ni 'uchunguzi wa hali na athari za mbinu tofauti za shughuli za kijamii na utafiti unaoleta utendaji wa kijamii'. Utafiti wa aina hii unafuata msururu wa hatua, kila moja ikiwa na utaratibu, shughuli na utafutaji wa ukweli kuhusu matokeo ya shughuli husika'. 'Utafiti tendaji ni jaribio, na unahusisha utekelezaji wa shughuli ili kutalii athari zake.' (Hall et al., n.d.).

**Uwezo wa ujirekebishaji:** Uwezo wa mifumo, taasisi, watu na viumbe wengine kujirekebisha ili kukabili madhara yanayoweza kutokea, kuitumia fursa au kukabiliana na athari (IPCC, 2018).

**Uanuwai wa viumbe:** Uanuwai wa viumbe wadogo, mimea na wanyama ulimwenguni au katika eneo maalum. Inajumuisha pia uanuwai wa kijeni na uanuwai wa mifumo ya ikolojia - yaani, mitagusano tofauti baina ya viumbe, hewa, maji, na udongo. Uanuwai mkubwa wa mimea na wanyama unaashiria mazingira bora.

**Mabadiliko ya Tabianchi:** Ni mabadiliko ya kilimwengu katika ruwaza za hali ya hewa katika kipindi kirefu cha wakati. Mabadiliko haya yanaweza kusababisha hali ya hewa ambayo ni hatari kama vile mafuriko na kiangazi au kuzidisha masuala mengine kama vile uharibifu wa radhi na ukataji miti.

**Uhifadhi:** NI tendo la kutunza, kukinga, kulinda na kutumia mazingira kwa uendelevu, ikiwemo kwa uanuwai wa viumbe na kudumisha mali asili na afya ya mfumo wa ikolojia.

**Mfumo wa ikolojia:** Ni mtandao changamano wa vipengele vya kibiolojia, ikiwemo jumuiya za viumbe walio hai (mimea, wanyama, ndege, samaki, na viumbe wadogo), na jinsi viumbe hawa wanaingiliana wao wenyewe na wanavyoingiliana na mazingira yao - ikiwemo hewa, maji, nuru ya jua na udongo.

**Huduma za mfumo wa ikolojia**: Uwezo wa mazingira kutoa manufaa (kama vile hewa safi, maji, chakula, oksijeni, rutuba ya udongo, uanuwai wa viumbe na virutubisho) kwa manufaa ya binadamu na kutoa maisha bora.

**Mandhari:** Sifa za asili na za kimaumbile za ardhi, pamoja na hewa na maji. Mandhari ni dhana jumuishi ambayo inatumiwa kurejelea kikundi cha rasilimali (udongo, uoto, njia za maji, vinamasi, uanuwai wa viumbe na kadhalika) katika eneo la kijiografia. Inajumuisha pia amali za binadamu (kwa mfano, jamii, miundomsingi na utawala). Mipaka ya eneo la kijiografia inaweza kubainishwa kwa sifa za kibiolojia na maumbile na/au sifa za utambuzi/shirikishi lakini mara nyingi inahusishwa na 'chanzo' au maeneo/ vipengele ambavyo vinashiriki sifa fulani za mandhari.

**Ukuaji upya:** ni sehemu ya Urejesho ambayo inajikita kwa ukuaji upya wa mimea kupitia visiki vilivyo hai ('misitu iliyo chini ya ardhi').

**Urejesho**: Mchakato wa kurudisha kitu katika hali yake nzuri ya hapo awali. Urejesho wa mfumo wa ikolojia au kimazingira ni mchakato wa kudhibiti uharibifu wa mifumo ya ikolojia ili kuboresha uzalishaji na uwezo wake wa kukidhi mahitaji ya jamii.

# 1. UTANGULIZI

Mazingira asili ni kipengele muhimu kwa maisha ya binadamu. Ingawa hakuna mtu yeyote duniani ambaye anaweza kujitenga kikamilifu na mali asili, watu wawili kati ya watatu katika nchi za kitropiki kote barani Afrika, eneo la Pasifiki ya Asia, na Amerika hutegemea moja kwa moja mali asilia kwa maisha yao: kama chanzo cha chakula, maji ya kunywa, nishati, nyenzo za makazi na mengi zaidi (Fedele et al., 2021). Kutegemea pakubwa mali asili huwafanya wawe katika hatari kubwa ya uharibifu wa mazingira hasa kutokana na mabadiliko ya tabianchi, matumizi mabaya ya mali asili (k.m. Ukataji wa miti) na matumizi ya ardhi yasiyo na uendelevu. Mandhari yaliyoharibiwa huzuia jamii kukuza chakula cha kutosha, kupata maji au kufikia kuni. Jamii hizi pia zimo katika hatari zaidi kutokana na majanga yanayohusishwa na tabianchi na mizozo inayohusu mali asili. Hali hii huathiri kwa njia hasi uwezo wa jamii husika wa kuwa na maisha endelevu, na kusababisha idadi kubwa zaidi ya jamii dhaifu pamoja na familia na watoto walio hatarini. (World Vision International, 2023).

Kukabiliana na kudhibiti uharibifu wa ardhi ni muhimu katika kuhakikisha maisha ya baadaye ambayo ni salama na endelevu kwa jamii za mashambani. Kote duniani, jamii hizi zinabadilisha maisha yao na ardhi yao kupitia matumizi ya Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR). FMNR ni dhana, mwelekeo na mbinu ya kuwasaidia watumiaji wa ardhi wanaotegemea ulimwengu asili (jamii, familia, watu) kuvunja mnyororo wa usimamizi wa mali asili usio na uendelevu, uharibifu wa ardhi na hali za maisha zinazozidi kuzorota (k.m., ongezeko la umasikini, uhaba wa chakula). FMNR inakuza njia asili ya urekebishaji wa mandhari kwa kujikita kwa uteuzi, ulinzi na upogoaji wa vichaka vya miti iliyo na mizizi hai kiutaratibu. Kwa njia hii, FMNR ni suluhu ya nafuu ambayo inahitaji ufamahu mdogo sana au stadi za kiufundi na kwa jinsi hiyo ni chaguo linalowezekana hata kwa watumiaji wa ardhi wenye uhaba wa rasilimali, kama vile wakulima masikini walio hatarini, jamii za wafugaji na Wataalamu wa misitu. Inaweza kutumiwa katika mandhari tofauti (k.m., ardhi ya kulima, ardhi ya kufuga, ardhi ya misitu) na ni njia yenye athari chanya kwa mazingira, kama vile ongezeko la miti na uoto, kuimarika kwa hali ya hewa katika sehemu maalum na muundo wa udongo. FMNR inachangia mazingira bora yenye hali nzuri kwa uzalishaji wa kilimo cha bustani, ufugaji wanyama, usimamizi wa misitu na mbinu mseto za ukulima.

Katika jamii nyingi zinazotegemea mazingira asili, hasa zile zinazoathiriwa zaidi na uharibifu wa ardhi, ukataji wa miti na mabadiliko ya tabianchi, mbinu ya FMNR na mwelekeo wake wa kiutaratibu na wa kina bado ni mpya au haijulikani. Hivyo basi, kuleta mbinu ya FMNR katika jamii kunahitaji nafasi za kujifunza kuihusu, kutafakari na kufanya mazoezi ya hatua za kiufundi za FMNR (tazama Somo la 3.2). Hii aghalabu hufanyika katika warsha ya mafunzo ya kinadharia pamoja na maonyesho ya kiutendaji ya FMNR (k.m., katika shamba la maonyesho la kibinafsi au la jamii).

Licha ya nyenzo anuwai za mafunzo zilizopo kuhusu FMNR (kutoka kwa World Vision na watekelezaji wengine wa FMNR), hakuna rasilimali za kutekeleza mafunzo kwa watumiaji wa FMNR wanaotarajiwa. Nyenzo zinazopatikana zimejikita kwa mwongozo wa hali ya juu, huku kukikosekana mwongozo wa kina wenye dhana ya utondoti ya mafunzo (Kiambatisho A), miongozo ya uwezeshaji na nyenzo za kujifunzia. Mwongozo huu umeandaliwa ili kujaza pengo hili na kuwa kitabu cha marejeleo kwa hadira tatu kuu:

- waelekezi wanaoendesha mafunzo ya FMNR kwa watumiaji wa FMNR wanaotarajiwa
- washikadau wa kiufundi wanaohusika katika utekelezaji wa uingiliaji wa FMNR
- wote walio na ari ya kujifunza zaidi kuhusu dhana na mwelekeo wa FMNR.

Baada ya sehemu hii ya utangulizi (sehemu ya 1), mwongozo umepangwa ifuatavyo:

**Sehemu ya 2** inatoa malengo ya mwongozo na hadhira inayolengwa

**Sehemu ya 3** inatoa maelezo ya mwelekeo wa ufunzaji unaopendekezwa katika kuendesha warsha hii.

**Sehemu ya 4** inatoa mwongozo kuhusu ukubwa na muundo wa kikundi cha washiriki wa mafunzo, namna ya kutambua na kuteua mahali panapofaa na jinsi ya kupanga ratiba ya warsha.

**Sehemu ya 5** ndiyo sehemu kuu ya mwongozo huu. Inajumuisha vitengo vinne vya mafunzo vilivyopangwa katoka masomo kadhaa ambayo yanajumuisha maelekezo ya kina kwa wawezeshaji, pamoja na nyenzo za ujifunzaji zinazohusika. Kitengo cha kwanza cha mafunzo ni utangulizi kwa warsha na mwelekeo wake. Kitengo cha pili kinatoa ufahamu wa kimsingi kuhusu uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili, na kinawahimiza washiriki kutafakari na kuelewa uhusiano wake. Mchakato huu unasaidiwa na nyenzo ya mchoro wa uhusiano ambao washiriki watajifunza jinsi ya kutumia. Katika kitengo cha tatu cha mafunzo, washiriki wanafahamishwa kwa dhana na mwelekeo wa FMNR na kuelewa mbinu zake za kiufundi, mchakato wa maendeleo ya jamii na upeo wa matumizi yake. Mwisho, kitengo cha nne, ambacho ni cha mwisho, kinahitimisha na kutathmini warsha, na kuwezesha washiriki kutafakari kuhusu yale wamejifunza.



# 2. AZMA NA WALENGWA WA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu unatoa muundo wa kina, maelekezo ya hatua baada ya hatua ya uendeshaji na maudhui ya kujifunza (ikiwemo nyenzo za ujifunzaji) kwa warsha ya kinadharia yenye muundo wa darasa kuhusu FMNR kwa watumiaji wa FMNR wanaotarajiwa kama vile wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Mbinu za kujifunza na maudhui yaliyobainishwa katika mwongozo huu yameandaliwa kutokana na mafunzo halisi ya FMNR na kufanyiwa majaribio katika miktadha tofauti ya mifumo ya ikolojia ya kilimo, uchumaji riziki na kitamaduni.1 Wakati wa kuendesha warsha hii, inapendekezwa kuichanganya na maonyesho ya kiutendaji kuhusu mbinu za kimsingi za FMNR katika shamba (tazama Somo la 3.2).

## 2.1 Mwongozo huu unalenga nani?

Mwongozo huu kimsingi unalenga wakufunzi washikadau ambao wanapanga kuendesha mafunzo kuhusu FMNR wakilenga watumiaji wa FMNR wanaotarajiwa kama vile wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Hii inajumuisha wafanyakazi wa kiufundi kutoka kwa mashirika ya serikali, taasisi za maendeleo ya umma, taasisi za Umoja wa Mataifa, mashirika ya ndani na ya kimataifa yasiyokuwa ya kiserikali, mashirika ya kijamii, utafiti wa taasisi za maendeleo (k.m. CGIAR - Kikundi cha Ushauri cha Utafiti wa Kilimo wa Kimataifa) na watekelezaji wengine wanaotarajiwa miongoni mwa washikadau wengine. Kwa jumla, mwongozo huu hauchukulii kwamba watumiaji wake wana ufahamu wa kiusuli kuhusu FMNR na kwa hivyo unawafaa Wataalamu wenye tajriba na wale wanaopanga mafunzo ya FMNR kwa mara ya kwanza. Isitoshe, mwongozo huu pia unaweza kutumiwa kama nyenzo ya kujifunza binafsi kuhusu FMNR.



*Mafunzo ya FMNR kwa Wakufunzi. © World Vision Kenya*

1 Mbinu za ufunzaji zimefanyiwa majaribio kwa jamii za wafugaji na za wakulima ambao shughuli zao za kutafuta riziki zinahusu ufugaji wa wanyama na kilimo cha mimea mtawalia. Mbinu hizi pia zimethibitishwa kuwa faafu kwa mandhari ya upandaji wa misitu, ardhi ya malisho na hata ya kilimo. Katika ardhi ya kilimo, miktadha kame na isiyo kame kabisa, mbinu za ufunzaji zimezalisha mabadiliko ya kufurahisha yenye uwezo mkubwa wa kudhibiti uharibifu wa mandhari.

## 2.2 Malengo ya mwongozo huu na warsha

Mwongozo huu ni stakabadhi elekezi yenye kina kwa wawezeshaji wa warsha kuhusu FMNR kwa watumiaji wa FMNR wanaotarajiwa. Maudhui yake yanajumuisha dhana ya mafunzo ya siku moja (Kiambatisho A), mfano wa ratiba ya warsha, masomo thabiti ya mafunzo (kila somo likiwa na taarifa za kiusuli na maelekezo ya uendeshaji pamoja na orodha ya rasilimali zinazohitajika) na muundo wa tathmini ya kujitathmini kabla na baada ya warsha kukadiria ufahamu unaohusika, stadi na mtazamo. Hivyo basi, mwongozo huu unalenga kuwapa wawezeshaji wa warsha taarifa yote muhimu, miongozo na rasilimali za kupanga, kusanifu, kuendesha na kutathmini warsha kuhusu FMNR kwa watumiaji wa FMNR wanaotarajiwa. Mwongozo huu pia unapendekeza chaguzi za jinsi ya kurekebisha muundo wa warsha kwa miktadha maalum.

Lengo la jumla la warsha ni kutanguliza jamii zinazotegemea ulimwengu asili na watumiaji wa ardhi kwa dhana na mbinu ya FMNR. Warsha inalenga vipengele vya ujifunzaji wa kinadharia vya FMNR na inapaswa kuunganishwa na maonyesho/mafunzo tendaji nyanjani. Lengo kuu la warsha ni kwamba washiriki:

- watajifunza kuhusu dhana ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili katika maisha yao binafsi na katika muktadha wa kazi.
- watajifunza na kutafakari juu ya FMNR kama mbinu ya urejesho wa mandhari ambayo ni ya kiasili, na gharama ya chini, kama sehemu ya mwelekeo endelevu wa usimamizi wa mali asili katika maisha yao binafsi na katika muktadha wa kazi.
- wataelewa vipengele tofauti vya FMNR na hatua muhimu za kuanzisha FMNR katika jamii na/au kaya
- wanafahamu manufaa ya FMNR kwa maisha yao binafsi na muktadha wa kazi katika maeneo ya mashambani.

Kimsingi, warsha inalenga kutoa jukwaa la kujifunza, kutafakari na kujadili juu ya FMNR na dhana zinazohusika kama vile uharibifu wa ardhi na ukataji wa miti. Washiriki wanapaswa kushiriki kiutendaji katika warsha na kuweza kusimamia na kudhibiti mchakato wao wa kujifunza (tazama pia Sehemu ya 3).



*Karisis (katikati) anatembelewa na marafiki wake na wenyeji wa Kaunti ya Narok nchini Kenya kupanda miti ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameathiri eneo hilo. © World Vision Kenya*

# 3. KANUNI ZA UFUNZAJI ZA WARSHA HII

Mbinu za ufunzaji katika warsha hii zimetolewa kwenye kanuni za kawaida za ufunzaji wa watu wazima 2 (tazama Jedwali la 1) na mwongozo uliopo wa uendeshaji wa warsha za FMNR kutoka World Vision. 3 Kwa hivyo, muundo wa warsha umejikita katika kanuni kadhaa za ufunzaji ambazo wawezeshaji wanaweza kushiriki na kukubaliana na washiriki mwanzoni mwa warsha hii (tazama Somo la 1.2).

***Jedwali 1: Kanuni za ufunzaji wa watu wazima na athari zake kwa mafunzo***

| Kanuni za ufunzaji wa watu wazima | Athari kwa ufunzaji |
|---|---|
| Watu wazima hujifunza vyema zaidi wanapohisi mafunzo kuwa ni faafu kwa mahitaji yao | • Toa 'mifano hai' na usisitize matumizi ya mafunzo kwa matatizo ya kweli.<br>• Tambua mahitaji ya wanafunzi na kile ambacho ni muhimu kwao |
| Watu wazima hujifunza kwa kutenda na kwa kuhusishwa kikamilifu katika mchakato wa kujifunza. | • Toa mazoezi ambayo yanahitaji ushiriki tendaji wa wanafunzi<br>• Toa mazoezi yanayohusisha wanafunzi wote kwa pamoja; mawazo yao, mitazamo, hisia na mwili |
| Watu wazima wana mitindo ya kipekee ya kujifunza; wanajifunza kwa njia tofauti, katika kasi tofauti na kutokana na tajriba tofauti | • Tumia mbinu anuwai za mafunzo<br>• Hakikisha kuna mazingira ya heshima na uelewe tofauti |
| Washiriki wanakuja kwenye mafunzo haya wakiwa na ufahamu na tajriba muhimu zifaazo | • Toa nafasi za kushiriki taarifa<br>• Jadili na uchanganue tajriba za washiriki<br>• Tumia washiriki kama rasilimali na uwahimize kuhusika na kushiriki tajriba zao. |

Kutoka: Fischer et al., 2019.

Kanuni hizi zinaweza kurekebishwa kwa mwongozo huu wa mafunzo ifuatavyo:

## Kanuni 1: Washiriki wanawajibikia ujifunzaji wao

Warsha ya FMNR imesanifiwa kama safari ya utambuzi inayojikita katika tafakari ya kibinafsi, majadiliano, na ujifunzaji wa pamoja. Jukumu la mwendeshaji sio sawa na la mhadhiri, lakini ni msimamizi anayewatambulisha washiriki kwa mitazamo mipya, mawazo na changamoto. Washiriki wanawajibikia ujifunzaji wao wakati wa warsha. Hii inamaanisha kwamba wawezeshaji wana uwazi kuhusu malengo ya somo na mbinu za kutumiwa katika warsha, huku pia wakitoa nafasi kwa washiriki kujiamulia malengo yao ya kujifunza (k.m., Somo la 1.3) na kushiriki tafakari, maswali na tajriba zao binafsi (k.m., kupitia fursa za mara kwa mara za maswali na majibu wakati wa somo au mwishoni mwa kila somo). Ingawa washiriki wanawajibikia kushiriki kiutendaji katika warsha hii, wawezeshaji pia wanastahili kupanga mazingira faafu na kuelekeza majadiliano kwa umakinifu ili kuhakikisha kwamba warsha inasalia ndani ya mipaka ya malengo yake na inajikita katika kufikia lengo lililoazimiwa (tazama Somo la 4.1 na 4.2).

2 Kwa taarifa zaidi, tafadhali rejelea sura ya 2 ya International Institute of Tropical Agriculture's Gender analysis in farming systems and action research: Mwongozo wa mafunzo, https://cgspace.cgiar.org/items/ef277e44-67d1-4bd0-b506-475490558d14.

3 Tazama World Vision Australia's FMNR Workshop: Maelekezo kwa wawezeshaji, http://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2014/06/FMNR-Workshop-Facilitator- Guidelines.pdf.

## Kanuni 2: Kuheshimiana

Kuheshimiana ni hitaji muhimu kwa ujifunzaji wenye ufanisi wakati wa warsha hii. Kanuni hii inarejelea kuheshimiana baina ya wawezeshaji wa warsha na washiriki pamoja na kuheshimiana miongoni mwa washiriki wenyewe. Mtazamo chanya unahitajika ili kuwatia moyo washiriki kuzungumzia shauku zao za kibinafsi, tajriba na maswali yao, na kuwezesha majadiliano bora na ujifunzaji.

## Kanuni 3: Mseto wa miundo tofauti ya kujifunza

Watu wana mitindo ya kipekee ya kujifunza na huelekea kupendelea miundo na mbinu tofauti za kujifunza. Hii inamaanisha kwamba wawezeshaji wanastahili kuchanganya mbinu tofauti za kujifunza (k.v. Mihadhara, kazi ya vikundi, mazoezi ya kibinafsi) na nyenzo tofauti. Kila inapofaa, wawezeshaji wanaweza kutumia video fupi katika hatua maalum.

## Kanuni 4: Tafakari kuhusu hatua za kujifunza

Tafakari ya mara kwa mara kuhusu hatua ya kujifunza wakati wa warsha husaidia kuelewa ufaafu wa muundo wa warsha. Pia huwasaidia wawezeshaji kushughulikia mahitaji maalum na mapendeleo ya kikundi maalum katika warsha. Wawezeshaji kwa hivyo wanahimizwa kuendesha tathmini fupi mwanzoni na mwishoni mwa warsha hii (tazama Somo la 1.4 na 4.1), kujumuisha kipindi kifupi cha kutamatisha maudhui na mafunzo muhimu katika hatua mahususi za warsha, na kuruhusu washiriki kuuliza maswali na kutoa majibu. Ni muhimu kuhakikisha kwamba wawezeshaji wanazingatia muda ulioratibiwa kwa warsha hii.

## Kanuni 5: Mahusiano

Washiriki wa warsha wanatarajiwa kutumia warsha hii kutangamana na kujenga mahusiano na washiriki wengine. Wawezeshaji wanaweza kuibua wazo la kubuni mtandao (k.m., Kikundi cha WhatsApp) na kuwahimiza washiriki kutangamana na kupanga mahusiano ya baada ya warsha hii.



# 4. MASUALA YA MSINGI YA WARSHA YA FMNR

Sehemu hii inaangazia vipengele vichache ambavyo wawezeshaji wa warsha wanashauriwa kuzingatia katika hatua ya kupanga warsha hii. Hii inajumuisha kubainisha ukubwa na muundo wa kikundi, kutambua na kuteua eneo faafu, na kupanga ratiba ya warsha.

## 4.1 Ukubwa na muundo wa kikundi

Wakati wa kupanga warsha kuhusu FMNR, ni muhimu kuzingatia ukubwa na muundo wa kikundi cha washiriki. Warsha iliyowasilishwa katika mwongozo huu inahimiza ushiriki tendaji, hivyo basi ukubwa wa muundo wa kikundi unapaswa kuamuliwa ili kila mshiriki ashiriki kikamilifu katika warsha hii. Katika kuandaa warsha hii, wawezeshaji wanapaswa kutafakari kuhusu vipengele na utaratibu unaowezekana wa kuamua ukubwa na muundo wa kikundi cha washiriki ili kuruhusu ushiriki tendaji wakati wa warsha.

Katika kushughulikia ukubwa wa kikundi, warsha imeendeshwa kwa vikundi vya baina ya washiriki 20 hadi 30. Hata hivyo, ukubwa wa kikundi unaweza kutofautiana kutegemea muktadha wa mafunzo (k.m., kutoa mafunzo kwa kikundi kinachoshiriki shughuli sawa kama vile kikundi cha uzalishaji wa bidhaa fulani), bajeti iliyopo, muda na waendeshaji. Kwa jumla, ushiriki tendaji unaelekea kuwa rahisi katika vikundi vidogo, huku vikundi vikubwa aghalabu vikidhibiti upeo wa ushiriki wa moja kwa moja wa washiriki wote.




*Washiriki wa mafunzo ya FMNR na Mwezeshaji. © World Vision Ethiopia*

Muundo wa kikundi cha warsha unaweza kutofautiana katika miktadha tofauti na kutegemea azma za mafunzo. Kwa kuwa uanzishaji wa FMNR ni mchakato unaojikita katika jamii, inapendekezwa kuhakikisha kwamba vikundi muhimu vya kijamii na njia za kujikimu (k.m., wakulima, wafugaji, na Wataalamu wa misitu) katika jamii maalum wanawakilishwa katika warsha hii. Hii pia inajumuisha uwakilishi sawa baina ya wanawake na wanaume. Kwa wakati huo, waendeshaji wa warsha wanastahili kuzingatia mahusiano hasi katika kikundi kutokana na ukosefu wa usawa wa kiuwezo au mbinu za kitamaduni (k.m., kulingana na jinsia, umri, hadhi ya kijamii, hali ya maisha kiuchumi). Kila inapowezekana, wawezeshaji wanapaswa kupanga vikundi vya warsha katika njia ambayo inapunguza hatari ya mahusiano hasi katika kikundi

**Kisanduku cha mazingatio ya wawezeshaji**

- ✓ Je, umewajumuisha watu kutoka vikundi muhimu na usuli wa kiuchumi katika kikundi cha warsha?
- ✓ Je, umebainisha vigezo bayana kuhusu ukubwa na muundo wa kikundi ambao unawezesha na kuruhusu ushiriki tendaji wa kila mshiriki?
- ✓ Je, ukubwa wa kikundi unaruhusu kila mshiriki kuhusika kikamilifu katika warsha hii?
- ✓ Je, umezingatia athari hasi katika kikundi na ukosefu wa usawa wa kiuwezo (k.m., kuhusu jinsia, umri, hadhi ya kijamii, hali ya maisha kiuchumi) ambayo inaweza kuzuia ushiriki tendaji?

## 4.2 Mahali pa warsha

Warsha inaweza kuendeshwa katika maeneo tofauti. Katika hali nyingi, eneo la warsha kwa kiasi kikubwa litategemea hali za ndani katika muktadha husika. Katika siku za hapo mbeleni, mafunzo yameweza kuendeshwa katika majengo ya umma, (k.m., shule, vituo vya kijamii, vituo vya vijana, kanisa) pamoja na maeneo ya wazi kama vile mabarazani, sokoni na mahali pengine pa mikutano. Ingawa hii ni mifano ya maeneo yanayowezakana kufanyia warsha, ni muhimu kuhakikisha kwamba mahali palipochaguliwa panatimiza vigezo fulani vya kimsingi.

Wawezeshaji wa warsha wanastahili kuzingatia vipengele vifuatavyo, wanapoteua mahali faafu pa kuendeshea warsha:

- **Ufikikaji:** Ni muhimu kuteua mahali ambapo panaweza kufikiwa kwa urahisi na washiriki wote. Ingawa hii huenda ikawa ni ufikiaji hali au wa kijamii, wawezeshaji wa warsha wanapaswa pia kuzingatia aina tofauti za usafiri na vizuizi vingine vya ufikiaji au vikundi tofauti vya washiriki (k.m., wanawake, wanaume, vijana, wakongwe, watu wenye ulemavu). Umbali wa mahali pa warsha kutoka kwa kundi lengwa pamoja na usafiri wa washiriki unapaswa kuzingatiwa ili kuruhusu ufikaji kwa wakati na salama (kanuni ya 'kutoleta madhara'6) na kuondoka kutoka kwenye warsha. Changamoto za ufikiaji wa mahali pa warsha zinaweza kusababisha watu kutofika au kukosa kushiriki.
- **Kazi ya vikundi:** Mahali pa warsha panapaswa kuruhusu uendeshaji wa mazoezi katika vikundi vidogo. Hii inahitajika ili kutoa mazingira faafu kwa baadhi ya masomo (tazama Sehemu ya 5). Wawezeshaji wa warsha kwa hivyo wanapaswa kuhakikisha kwamba kazi ya vikundi inaweza kufanyika katika mahali pa warsha.

.

.

4 Unapopanga kipindi kimoja tu cha mafunzo katika jamii, uwakilishi wa vikundi tofauti vya kijamii na kiuchumi ni muhimu, licha ya ongezeko la athari hasi katika kikundi, kwa kuwa vikundi vyote vinastahili kufikiwa wakati wa mafunzo. Katika hali ambapo mafunzo kadhaa ya FMNR yanaendeshwa katika jamii moja, wawezeshaji wanaweza kutafakari manufaa ya kutenganisha mafunzo kwa wanawake na wanaume pamoja na vikundi tofauti vya watumiaji wa ardhi (k.m., wakulima, wafugaji, Wataalamu wa misitu). Fursa ya ushiriki tendaji katika warsha inapaswa kuwa kanuni ya msingi katika hali yoyote ile.

5 Hii pia ni muhimu wakati wa kuunganisha mafunzo ambayo yanatenga washiriki kutoka jamii tofauti. Katika hali hii, ikiwa haitazingatiwa kwa makini, umbali wa mahali pa warsha pamoja na masuala ya kijamii yanaweza kuzuia ushiriki wa baadhi ya washiriki.

6Kanuni ya 'Kutoleta Mdhara' ni dhana au mwelekeo wa kufanya mipango na kuitekeleza kwa kuzingatia mizozo kila inapohusika. Matokeo hasi na athari zisizotarajiwa za ushirikiano wa maendeleo na msaada wa kibinadamu zinapaswa kutambuliwa, kuepukwa na kushughulikiwa katika hatua za mapema.

- **Hali za kujifunza:** Inapendekezwa pia kuendesha warsha katika mahali penye utulivu ili kuepuka ukatizaji kutoka nje na kutoa mazingira faafu kwa ujifunzaji.

**Kisanduku cha mazingatio ya wawezeshaji**

- ✓ Je, mahali pa warsha pameteuliwa kwa kuzingatia wepesi wa ufikiaji kwa washiriki wote?
- ✓ Je, umezingatia vizuizi vya usafiri tofauti (vizuizi halisi na vya kijamii) kwa vikundi tofauti vya ushiriki kama vile wanawake, wanaume, vijana na wakongwe?
- ✓ Je, mahali pa warsha panafaa kwa uendeshaji wa kazi ya vikundi?
- ✓ Je, mahali pa warsha pana mazingira yenye utulivu?

## 4.2 Ratiba ya warsha.

Dhana ya warsha na ratiba iliyopo katika mwongozo huu kwenye Jedwali 2 imeandaliwa kutokana na mafunzo mbalimbali ya FMNR katika miktadha tofauti. Muundo na maudhui ya mwongozo huu yameandaliwa kuambatana na mfano wa ratiba uliotolewa. Ratiba hii imebainishwa kuwa na ufanisi katika kutanguliza FMNR kwa kikundi kipya cha watumiaji wanaotarajiwa na kuibua majadiliano na tafakari kuhusu usimamizi wa mazao ya miti na mali asili nyingine katika jamii. Kwa wakati huo huo, ratiba ya warsha na yaliyoelezwa hapa chini yamezingatiwa kuwa pendekezo la ratiba, ambayo watumiaji wa mwongozo huu wanaweza kurekebisha kulingana na azma ya mafunzo na kundi lengwa. Ratiba ya warsha hivyo basi haipaswi kuchukuliwa kama isiyoweza kubadilika na inaweza kurekebishwa kuafiki mahitaji maalum.

*Jedwali 2: Kielelezo cha ratiba ya warsha*

| Muda | Kitengo/Somo |
|---|---|
| **08:30–09:00** | Usajili |
| | **Kitengo 1 cha ujifunzaji: Ufunguzi wa warsha** |
| **09:00–09:15** | 1.1 Makaribisho na utangulizi |
| **09:15–09:20** | 1.2 Kanuni na sheria za ufunzaji za warsha hii |
| **09:20–09:30** | 1.3 Maudhui ya warsha na malengo ya somo |
| **09:30–09:45** | 1.4 Tathmini ya kabla ya warsha |
| *Mapumziko ya Chai* | |
| | Kitengo 2 cha ujifunzaji: Uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili |
| **10:00–11:15** | 2.1 Michoro ya uhusiano ya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili |
| **11:15–11:45** | Masuala ya msingi kuhusu uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili |
| **11:45–12:15** | 2.3 Utangulizi kwa Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) ) |
| *Chamcha* | |

| | |
|---|---|
| | Kitengo 3 cha ujifunzaji: Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR) |
| **13:00–14:00** | 3.1 Utangulizi kwa FMNR |
| **14:00–14:15** | 3.2 FMNR kama mbinu ya kiufundi |
| **14:15–14:45** | 3.3 FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii |
| **14:45–15:15** | 3.4 Upeo wa kutumia FMNR |
| | ***Mapumziko ya Chai*** |
| | Kitengo 4 cha ujifunzaji: Kufunga warsha |
| **15:30–16:15** | 4.1 Hitimisho na tathmini baada ya warsha |
| **16:15** | Mwisho wa warsha |



# 5. VITENGO VYA UJIFUNZAJI NA MASOMO

Sehemu hii ndiyo kubwa katika mwongozo huu wa warsha ya FMNR. Inajumuisha maelezo ya kina ya vitengo vinne vya ujifunzaji. Kila kitengo cha ujifunzaji kinajumuisha masomo kadhaa. Mwanzoni mwa kila somo, kuna jedwali la muhtasari linalotoa maelezo kwa mwezeshaji kuhusu makadirio ya muda, malengo ya somo na mada. Aidha, inajumuisha taarifa muhimu katika hatua ya maandalizi (k.m., maandalizi ya nyenzo na mbinu za kutumia). Muhtasari huu unapaswa kuwasaidia watumiaji wa mwongozo huu kuelewa kwa haraka masuala muhimu na mazingatio ya somo husika. Maagizo ya kina na maelekezo ya kumsaidia mwezeshaji katika utekelezaji wa somo. Masomo manne ambayo yanaangazia dhana na mbinu za FMNR (katika kitengo 2 na 3 cha ujifunzaji), usuli wa kinadharia na mapendekezo ya usomaji wa ziada yametolewa kumsaidia mwezeshaji kujiandaa kwa warsha. Isitoshe, masomo mengi yanajumuisha sehemu za ziada zinazoitwa 'Taarifa kwa Mwezeshaji,' ambazo zinatoa muhtasari wa jumla na maoni yanayotokana na tajriba ili kumsaidia mwezeshaji katika kuendesha warsha.

## Kitengo 1 cha ujifunzaji: Ufunguzi wa warsha

Kitengo cha kwanza cha ujifunzaji kinasheheni masomo manne: (1) kipindi cha makaribisho na Utangulizi, (2) uwasilishaji wa sheria za ufunzaji zitakazozingatiwa katika warsha (3) utangulizi wa maudhui ya warsha na malengo ya somo, na (4) tathmini ya kabla ya warsha.

*Mchoro 1 Kitengo 1 cha ujifunzaji: Ufunguzi wa warsha*

**Somo la 1.1: Makaribisho na utangulizi**

Somo la kwanza ni la wawezeshaji wa warsha kuwakaribisha na kuwatambulisha washiriki kwa sababu ya jumla ya kuwa na warsha na shabaha yake kimaudhui. Washiriki na wawezeshaji wanapata kufahamiana kwa kuwa washiriki wanapewa nafasi ya kujitambulisha.

**Somo la 1.2: Kanuni na sheria za ufunzaji za warsha hii**

Katika somo hili, wawezeshaji hueleza kanuni za ufunzaji wa warsha hii na masharti ya mienendo, ambayo yamejikita kwenye kanuni za jumla za ujifunzaji wa watu wazima..

**Somo la 1.3: Maudhui ya warsha na malengo ya somo**

Katika somo la tatu, wawezeshaji wa warsha wanatoa muhtasari wa upeo na maudhui ya warsha na malengo ya somo kwa washiriki. Kupitia kwa zoezi shirikishi, washiriki wanaombwa kueleza na kushiriki matarajio yao na malengo ya somo
.

**Somo la 1.4: Tathmini ya kabla ya warsha**

Kama somo la mwisho la kitengo hiki, wawezeshaji wanasambaza fomu za tathmini ya kibinafsi kwa washiriki ili wajaze kabla na baada ya mafunzo yenye maswali yanayohusu maudhui ya warsha na masomo.

# Somo la 1.1: Makaribisho na utangulizi

*Jedwali 3: Somo la 1.1 muhtasari*

| Muhtasari | Makaribisho na utangulizi |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 15 |
| **Malengo ya Somo** | ➢ Washiriki watajua shabaha kuu ya kimaudhui ya warsha hii<br>➢ Na wawezeshaji wa warsha wanapata kufahamiana |
| **Mada** | ◊ Makaribisho<br>◊ Kufahamiana |
| **Maandalizi** | ❋ Andaa ukurasa wa makaribisho kwenye chati<br>❋ Kabla ya washiriki kufika, panga viti kwa umbo la nusu duara kwa ajili ya kipindi hiki cha utangulizi |
| **Nyenzo** | ☼ Chati<br>☼ Kalamu za Kuandikia Ubaoni |
| **Mbinu** | ∗ Mawasilisho<br>∗ majadiliano ya pamoja |
| **Maelekezo** | ✓ Hakikisha kila mmoja amejitambulisha |

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

**Hatua ya 1:** Andaa kipindi kwa kuwaalika washiriki kuketi kwenye viti vilivyopangwa katika umbo la nusu duara. Wakaribishe, jitambulisha na uwaruhusu wawezeshaji wengine kujitambulisha. Ikiwa kuna shirika lililowakilishwa, mwalike mwakilishi wao (ikiwa yupo) afungue warsha.

**Hatua ya 2:** Eleza sababu ya jumla na shabaha ya kimaudhui ya warsha hii. Ikiwa warsha inaendeshwa chini ya mfumo wa mradi, eleza usuli wa mradi huo kwa muhtasari.

**Hatua ya 3:** Kwa kuzingatia muktadha wa kitamaduni na ukubwa wa kikundi, mwalike kila mshiriki kujitambulisha kwa kifupi (jina, nyumbani, jamii, n.k.). Waombe washiriki waendelee mmoja baada ya mwingine.

**Hatua ya 4:** Washukuru washiriki baada ya wao kukamilisha kujitambulisha na uendelee kwenye somo la pili.

### Maagizo kwa mwendeshaji:

- Kutegemea muktadha wa kitamaduni wa kikundi husika, unaweza kujumuisha kipindi kifupi cha maombi katika ratiba. Unaweza kuuliza ikiwa mshiriki yeyote angependa kuongoza maombi hayo.
- Katika kujitambulisha, unaweza kumuomba kila mshiriki kutaja jambo ambalo hakuna mtu anayejua ili kuwasaidia kutulia na kutangamana bila wasiwasi wakati wa warsha.
- Unaweza kuandika taarifa za kimsingi ambazo washiriki wanahitajika / wanatarajiwa kujumuisha katika kujitambulisha (k.m., jina, shirika/mahali, uzoefu wa FMNR, n.k.) kwenye chati kama itawezekana.

# Somo la 1.2: Kanuni na sheria za ufunzaji za warsha hii

*Jedwali 4: Somo la 1.2 muhtasari*

| Muhtasari | Kanuni na sheria za ufunzaji za warsha hii |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 15 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki wanafahamu kanuni za kimsingi za ujifunzaji zitakazotumiwa katika warsha hii.wanafahamu masharti ya kimsingi ya mienendo wakati wa warsha |
| **Mada** | Kanuni na sheria za ufunzaji |
| **Maandalizi** | Andaa kazi zenye kanuni na sheria za kimsingi za ufunzaji na uzipachike kwenye chati (inaweza kutundikwa ukutani mwa chumba cha mafunzo) |
| **Nyenzo** | Chati za Karatasi<br>Kadi<br>Kalamu |
| **Mbinu** | Mawasilisho<br>Majadiliano ya pamoja |

### Hatua na maagizo ya uwezeshaji

**Hatua ya 1:** Tanguliza kanuni na sheria za kimsingi za ufunzaji zitakazotumiwa katika warsha hii, k.m., ujifunzaji wa pamoja na wa uzoefu, tafakari na mahusiano. Eleza kanuni na kufafanua kwamba kuzifuata kutasaidia kuwezesha mbinu za ushiriki tendaji ambazo zinatumia tajriba na mitazamo ya washiriki.

**Hatua ya 2:** Waulize washiriki iwapo wako na maswali yoyote au maoni yanayohusiana na kanuni na sheria hizi na utoe majibu (ikiwa itahitajika). Ikiwa washiriki wangependa kuongezea kanuni au sheria za ziada kwenye orodha iliyopendekezwa, ziandike kwenye kadi na uzibandike kwenye chati. Kubaliana na washiriki kuhusu kanuni za ufunzaji.

**Hatua ya 3:** Funga somo na uendelee kwenye somo linalofuata.

### Maagizo kwa mwendeshaji:

- Kuwasilisha kanuni za ufunzaji husaidia kutanguliza dhana ya mazingira ya ufunzaji ambapo upimaji na majaribio yanaweza kufanyika kwa ufanisi. Hii inaendana na kuchukulia 'makosa' kama fursa ya kujifunza (tazama sehemu ya 3).

# Somo la 1.3: Maudhui ya warsha na malengo ya somo

*Jedwali 5: Somo la 1.3 muhtasari*

| Muhtasari | Maudhui ya warsha na malengo ya somo |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 15 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki<br>➢ wanafahamu upeo na maudhui ya warsha hii<br>➢ wameshiriki malengo na matarajio ya somo (ikiwa inahusika)<br>➢ na wawezeshaji wa warsha wamekubaliana kuhusu malengo ya somo ya warsha. |
| **Mada** | ◊ Upeo na maudhui<br>◊ Malengo ya Somo |
| **Maandalizi** | ❖ Andaa chati yenye muhtasari wa upeo na maudhui ya warsha<br>❖ Andaa chati yenye muhtasari wa malengo ya somo ya washiriki<br>❖ Andaa chati yenye ratiba ya warsha |
| **Maandalizi** | O Chati za Karatasi<br>O Kalamu za Kuandikia Ubaonini<br>O Kadi<br>O Kalamu |
| **Mbinu** | ➢ Mawasilisho<br>➢ Mdahalo wa pamoja |

### Hatua na maagizo ya uwezeshaji

**Hatua ya 1:** Eleza azma ya somo hili, i.e, utangulizi wa maudhui ya warsha, malengo ya somo na ratiba.

**Hatua ya 2:** Wasilisha upeo na maudhui ya warsha hii

**Hatua ya 3:** Wape washiriki muda wa kutoa maoni na kuuliza maswali na uwaalike kuzungumzia matarajio yao na malengo ya somo. Washukuru washiriki kwa kutoa maoni yao.

**Hatua ya 4:** Eleza ratiba ya warsha. Ipitie pamoja na washiriki na mpate kukubaliana.

**Hatua ya 5:** Funga somo na uende kwenye somo la mwisho katika kitengo hiki.

### Maagizo kwa mwendeshaji:

- Wawezeshaji wanaweza kuandika maoni ya washiriki kuhusu malengo ya somo na matarajio kwenye kadi ambayo inaweza kubandikwa kwenye chati.
- Vinginevyo (pia kwa kuzingatia uwezo wa kusoma na kuandika), washiriki wanaweza kuandika michango yao wenyewe, ambayo inaweza kupangwa kuambatana na malengo yaliyowasilishwa.

## Somo la 1.4: Tathmini ya kabla ya warsha

*Jedwali 6: Somo la 1.4 muhtasari*

| Muhtasari | Tathmini ya kabla ya warsha |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 15 |
| **Malengo ya Somo** | • Washiriki wametathmini ufahamu wao na uwezo kuhusu FMNR kabla ya warsha hii |
| **Mada** | ◊ Tathmini ya kibinafsi kuhusu ufahamu na uwezo wa awali kuhusu FMNR |
| **Maandalizi** | ▪ Andaa hojaji ya tathmini ya kabla ya warsha<br>▪ Kabla ya mafunzo, chapisha nakala ya fomu ya tathmini ya kabla ya warsha kwa kila mshiriki (Kiambatisho B) |
| **Nyenzo** | o Tathmini ya kabla ya warsha<br>o Kalamu |
| **Mbinu** | ➢ Fomu ya tathmini/Hojaji |
| **Maelekezo** | ❖ Washiriki ambao uwezo wao wa kusoma na kuandika unakwaza kuelewa na kujaza fomu hii wanapaswa kusaidiwa na wawezeshaji wa kipindi hicho |

### Hatua na maagizo ya uwezeshaji

**Hatua ya 1:** Wasilisha hojaji ya tathmini ya kabla ya warsha kwa washiriki ili kutathmini ufahamu na maarifa waliyo nayo kuhusu FMNR. Tathmini hii ya kibinafsi inawaruhusu washiriki kutambua umilisi wao, mapengo na mahitaji ya ujifunzaji mwanzoni mwa warsha. Fahamisha kikundi kwamba fomu sawa ya tathmini ya kibinafsi itasambazwa mwishoni mwa warsha. Hii itawaruhusu washiriki kutathmini maendeleo yao wenyewe na kukadiria ubora wa mafunzo. Sambaza hojaji za kwanza za tathmini ya kabla ya warsha.

**Hatua ya 2:** Kusanya hojaji washiriki wakikamilisha kuzijaza. Washukuru washiriki na ufunge kitengo cha kwanza

### Maagizo kwa mwendeshaji:

- Fomu ya tathmini binafsi inapaswa kuwa fupi na kulenga vipengele muhimu vya mafunzo.
- Ikiwa kuna washiriki wasio na uwezo wa kusoma na kuandika, mwezeshaji anapaswa kuwasaidia kujaza Hojaji ya kabla ya warsha.

## Kitengo 2 cha ujifunzaji: Uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili

Kitengo cha pili cha ujifunzaji kinajumuisha masomo matatu: (1) zoezi la tafakari shirikishi ya kikundi kuhusu dhana za uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili, kwa msingi wa tajriba na mitazamo ya washiriki; (2) utalii wa kinadharia wa dhana hizi tatu na mahusiano yake; na mwisho (3) utangulizi katika urejesho wa mandhari ya misitu. Katika kitengo hiki, washiriki wanatarajiwa kutafakari na kujadili uelewa wao wa uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili na kujifunza kuhusu  visababishi vyake, uunganifu na athari katika mazingira yao ya kiasili na ya kijamii na kiuchumi. Baada ya kukamilisha kitengo cha pili, washiriki wanaanza kuelewa uhusiano wa moja kwa moja baina ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na mikakati na mbinu za usimamizi wa mali asili za kuzuia na kukabiliana na athari hasi. Hii inaibua motisha ya awali ya kulinda mazingira yao na hivyo msingi wa kubadilisha mienendo na kukumbatia FMNR.

*Mchoro 2 Kitengo 2 cha ujifunzaji: Uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili*

**Somo la 2.1: Michoro ya uhusiano ya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili**

Katika somo hili, washiriki watatafakari vijenzi na vipengele vya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili katika miktadha ya maisha yao binafsi. Hii itafanyika kupitia kwa uchoraji wa mchoro wa uhusiano ambao unaruhusu kupata ruwaza ya vijenzi na vipengele pamoja na uhusiano wake. Michoro ya uhusiano itaonyesha jinsi washiriki wanachukulia uharibifu wa kimazingira na ukataji miti katika nyumba na jumuiya zao, vipengele ambavyo wanahusisha na dhana hizi mbili, na jinsi wanavyozielewa.

**Somo la 2.2: Masuala ya msingi kuhusu uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili**

Somo hili linahusisha utangulizi mfupi wa dhana hizi tatu na mahusiano yake makuu. Kila inapowezekana, wawezeshaji wa warsha watafanya viungo kwa matokeo kutokana na michoro ya uhusiano

**Somo la 2.3: Utangulizi kwa urejesho wa msitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii**

Katika kitengo hiki, washiriki wanatangulizwa kwa kifupi kwenye dhana ya urejesho wa  misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii. Lengo ni kwamba washiriki waelewe ulinzi wa miti na uoto kama suluhu inayowezekana kumaliza ukataji wa miti na uharibifu wa ardhi. Ili kutimiza azma hii, wawezeshaji wa warsha watawasilisha manufaa ya kimsingi kwa mazingira ya miti na uoto
Kwa hewa katika sehemu maalum, muundo na ubora wa udongo., na usimamizi wa maji.

## Somo la 2.1: Michoro ya uhusiano ya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili (zoezi la tafakari shirikishi katika kikundi)

### Usuli wa kinadharia

Mchoro wa uhusiano ni mbinu na nyenzo ya kimaelezo ambayo ni shirikishi na hutumiwa katika utafiti tendaji.

Inatoa taswira ya vipengele na vijenzi vya kigeu fulani au mada ya utafiti, pamoja na uhusiano wake.

Katika mafunzo haya, mchoro wa uhusiano umetumiwa kuwasidia washiriki kutafakari kuhusu mitazamo na uelewa wao wa dhana ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili, na kutambua masuala muhimu na vichocheo vinavyowiana. Shughuli hii inaweka msingi wa kuelewa mwelekeo wa FMNR.

### Vijenzi

Mchoro wa uhusiano hujumuisha vipengele kutoka fani mbalimbali (k.m., kijamii, kiuchumi, kiufundi, kimazingira) na katika viwango tofauti (k.m. Kibinafsi, familia, jamii). Isitoshe michoro ya uhusiano inalenga kutoa taswira na/au kuonyesha uhusiano baina ya vipengele maalum vinavyohusiana na mada moja au zaidi zinazoshughulikiwa. Uhusiano unaoonyeshwa katika mchoro huu unaweza kuwa wa aina tofauti, kama vile usababishaji, utegemezi na ukinzani. Hivyo basi mchoro wa uhusiano ni nyenzo ya uchanganuzi na ushiriki ambao unaruhusu washiriki kuonyesha ni vipengele vipi vinahusishwa na uharibifu wa kimazingira, ukataji wa miti na usimamizi wa mali asili.

### Mbinu ya mifumo

Mbinu ya mchoro wa uhusiano inajikita katika mitazamo ya mifumo ambayo inatambua uwepo na uhusiano wa vipengele tofauti vya mfumo. Hii inasaidia kutoa taarifa za kina kuhusu chanzo au visababishi vya matatizo katika mfumo ambao unazingatiwa. Kupitia kwa mweleko huu shirikishi, mchoro wa uhusiano unakuwa nyenzo ambayo inatimiza mahitaji ya warsha. Kwa kuwasaidia washiriki kutambua vipengele vinavyohusiana na uharibifu wa kimazingira, ukataji wa miti na usimamizi wa mali asili katika ngazi ya familia na jamii, nyenzo hii inakuza uchanganuzi hakikifu na mwelekeo wa kitaratibu, ambao unaweka msingi wa mabadiliko ya kimwenendo na kutoa nafasi za kuingiza FMNR. Ni kwa kuelewa na kushughulikia mfumo huu ambapo uingiliaji wa FMNR unaweza kutukia ndipo mabadiliko ya mfumo yanaweza kutokea.

### Uwezo wa warsha hii ya FMNR

Iwe mwezeshaji amefanya kazi na washiriki wa warsha hapo awali au ni mgeni katika uwanja huu, njia bora ya kuanza ni kuuliza wanajamii wanaohusika kile wanachojua kuhusu uharibifu wa kimazingira, na ukataji wa miti na shauku zao ni zipi. Matumizi ya mchoro wa uhusiano kwa hivyo unakuwa faafu kutimiza azma hii kwa kuwa:

» Unawaruhusu washiriki kutalii masuala ambayo ni ya shauku kuu kwao, kuunganisha na kulinganisha mitazamo mbalimbali

» Unasaidia kutambua vipengele vya kimsingi na visababishi vya mada husika, kama vile uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili

» Unawezesha tafakari na uelewa wa uharibifu wa mazingira, ukataji wa miti na usimamizi wa mali asili

» Unatoa kiingilio kwa mikakati na mbinu endelevu za usimamizi wa mali asili, ikiwemo FMNR.

### Kuchora mchoro wa uhusiano na washiriki wa warsha ya FMNR

Utekelezaji wa mbinu hii nyanjani unahusisha sehemu mbili kuu: (1) kuchora na kujadili mchoro wa uhusiano na kikundi kidogo cha washiriki (watu 3 hadi 5), na (2) uwasilishaji unaofuata na majadiliano ya pamoja ya michoro ya kila kikundi katika kikao jumuishi. Hii inaruhusu utangamano zaidi na tafakari miongoni mwa washiriki kuhusu michoro tofauti ya uhusiano inayotokana na mitazamo na tajriba tofauti (Campbell, 2002).

***Hatua za jumla katika kuchora na kujadili mchoro husika***

Zoezi la kuzalisha mchoro wa uhusiano linajumuisha hatua nne za jumla:

- Hatua ya 1: Kuteua shabaha
- Hatua ya 2: Kuchagua muktadha
- Hatua ya 3: Kuchora michoro ya uhusiano
- Hatua ya 4: Kutambua vipengele na vichocheo muhimu.

Katika hatua ya 1, kuna vibadala viwili vilivyoelezwa na vinavyotofautiana baina ya shabaha pana na shabaha finyu. Hii inaweza kubainishwa kulingana na shabaha inayolengwa na shughuli ya mchoro wa uhusiano na uanuwai wa washiriki. Hii inarejelea kuwa Hatua ya 1 (a) na Hatua ya 1 (b) hapa chini. Hakuna vibadala kama hivyo kwa hatua zilizosalia, ambazo zinapaswa kutumika kulingana na maagizo yaliyotolewa. Isitoshe, inapendekezwa kutumia lugha ambayo washiriki wanafahamu vyema zaidi na kutafsiri istilahi na dhana zinazotumika katika zoezi hili inavyostahili. Kwa jumla, zoezi lote halipaswi kuzidi zaidi ya dakika 60.

**Hatua ya 1(a): Kuteua shabaha pana**

Mwanzoni mwa shughuli, uamuzi unapaswa kufanywa kuhusu shabaha ambayo italengwa na mchoro wa uhusiano. Chaguo hili linatoa fursa ya kuchagua shabaha pana zaidi ambayo inalenga kushughulikia mada tatu za somo hili kwa pamoja: uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili. Dhana hizi mbili za uharibifu wa kimazingira na ukataji miti zinaweza kuhusishwa kwa karibu. Tafakari ya pamoja na majadiliano kuhusu dhana hizi mbili huenda ukawapa washiriki uelewa wa kina zaidi wa dhana hizi mbili, huku wakiangazia uhusiano wake. Mwelekeo huu unaweza kuchangia uelewa wa usimamizi wa mali asili kama mseto wa mikakati na mbinu ambazo zinazuia na/au kudhibiti vipengele vinavyohusishwa na uharibifu wa mazingira, na ukataji miti. Zaidi ya hayo, kuwa na shabaha pana kunaruhusu wanakikundi kueleza ufahamu wote wa aina tofauti, tajriba, na mitazamo katika uundaji wa michoro ya uhusiano.



**Hatua ya 1(b): Kuteua shabaha moja**

Chaguo lingine kwa hatua hii ya kwanza ni kuteua shabaha moja. Hii inamaanisha kwamba kila kikundi kinapaswa kulenga shabaha yake kwa dhana moja tu katika somo hili: (1) uharibifu wa kimazingira, (2) ukataji miti au (3) Usimamizi wa mali asili. Mwelekeo huu unaruhusu kushughulikia vipengele mahususi vinavyohusu dhana inayoangaziwa, na hivyo kuepuka taarifa ambayo ni ya jumla ambayo inaweza kujitokeza ikiwa shabaha pana imewekwa. Hii pia inaruhusu wanakikundi kutafakari kwa kina zaidi na kupata umaizi kuhusu vipengele vinavyohusiana na dhana maalum ambayo kikundi kimeombwa kushughulikia.

**Hatua ya 2: Kuchagua muktadha**

Mchoro wa uhusiano kila mara unalenga muktadha mahususi. Kama vipengele na vichocheo vya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na mikakati ya usimamizi wa mali asili hutofautiana katika maeneo na jamii tofauti, ni muhimu kuzingatia muktadha wa ndani ambao utaangaziwa na mchoro wa uhusiano. Wawezeshaji wanahitajika kuzingatia hili, kwa kuwa watakuwa wanatumia nyenzo sawa katika miktadha tofauti.

**Hatua ya 3: Kuchora michoro ya uhusiano**

Mchakato unaanza kwa kuandika jina la dhana hizi tatu (ikiwa ni Hatua ya 1 (a)) au dhana moja (ikiwa ni Hatua ya 1 (b)) katikati mwa bango. Hakikisha umesambaza majina kwenye chati hivi kwamba kuna nafasi ya kutosha kwa vipengele vinavyohusiana. Baada ya hapa, kikundi kitatafakari kwa pamoja na kujadili vipengele vyote vinavyohusiana na dhana inayohusika na kuzirekodi kwenye bango.

Uhusiano baina ya vipengele tofauti vimeonyeshwa kwa mistari au vishale. Kikundi kinapaswa kutumia muda kuandaa mchoro, kwa kuwa matokeo yatakuwa msingi wa kutambua vipengele muhimu na vichocheo vya uharibifu wa mazingira na ukataji wa miti, pamoja na mikakati na mbinu za usimamizi wa mali asili.

**Hatua ya 4: Kutambua vipengele na vichocheo muhimu**

Baada ya kukamilisha Hatua ya 3 mwezeshaji ataanzisha majadiliano ya kikundi katika vikundi vidogo vinavyohusika. Majadiliano yanapaswa kuangazia kukamilisha mchoro wa uhusiano kwa kutambua vipengele na vichocheo ambavyo ni muhimu zaidi na namna vinavyohusiana (k.m., Je, unaweza kueleza jinsi kipengele hiki kinahusiana na uharibifu wa kimazingira na/au ukataji wa miti? Je, unaweza kueleza kwa nini mkakati huu wa Usimamizi wa mali asili unadhibiti uharibifu wa kimazingira na/au ukataji wa miti?). Vikundi vidogo kisha hurudi katika kikundi cha pamoja na kila kikundi kidogo kitapewa nafasi ya kuwasilisha kwa kifupi na kueleza chati yao kwa washiriki wengine. Ili kuchochea majadiliano ya pamoja, mwishoni mwa kila wasilisho, washiriki wanaalikwa kuuliza maswali na/au kutoa maoni kuhusu mchoro wa uhusiano. Majadiliano haya yanasimamiwa na mwezeshaji.

**Kwa hiari:** Huenda ikawa muhimu kurekodi Zoezi la uchoraji ili kuakisi majadiliano, maamuzi na maoni katika hatua hii. Vinginevyo, shughuli hizi zinaweza kurekodiwa katika mfumo wa maandishi.



Mwezeshaji anaeleza mchoro wa uhusiano wakati wa mafnzo ya FMNR.
© World Vision Ethiopia

### *Je, nini kinahitaji kuzingatiwa katika kuteua wanachama katika kazi ya kikundi?*

Wakati wa kuunda kikundi ambapo kila mtu anahisi yuko sawa kushiriki kikamilifu na kutoa maoni yao wakati wa shughuli, ni muhimu sana kuzingatia kwa makini masuala ya kiuwezo baina ya washiriki wa warsha. Vikundi vilivyo na tofauti bayana za kijamii kama vile umri, jinsia, kiwango cha elimu na hadhi ya kijamii huenda vikazuia wanakikundi kushiriki kikamilifu. Wanawake hasa huenda wakapata ugumu kueleza maoni yao mbele ya wanaume. Kwa hivyo, inapendekezwa kuunda vikundi vinavyotenganisha jinsia kwa zoezi hili. Chaguo lingine ni kuteua washiriki kulingana na ilhamu za jumla (k.m. Kikundi cha wazalishaji, kikundi cha kuweka akiba, viongozi wa kijamii, walimu, n.k.). Kwa hivyo michoro shirikishi aghalabu huwa faafu zaidi inapotumiwa katika vikundi vyenye sifa zinazofanana, machaguo yote mawili yaliyopendekezwa yanaweza kuwaruhusu washiriki kuhisi wametulia katika kikundi na kuwa na mshawasha wa kushiriki kikamilifu katika zoezi hili.

### *Je, nini kinahitaji kuzingatiwa katika kuchagua mwezeshaji wa kazi ya kikundi?*

Katika hali ambapo kuna vikundi tofauti kijinsia, wawezeshaji wanapaswa kuwa wa jinsia moja kama washiriki (wawezeshaji wa kike kwa vikundi vya wanawake na wawezeshaji wa kiume kwa vikundi vya wanaume). Isitoshe, ili kupunguza upendeleo unaoweza kutokea kutokana na majukumu na mipangilio ya kijamii, itakuwa na manufaa ikiwa wawezeshaji hawatakuwa wanajumuiya wa jamii inayolengwa wala wafanyakazi ambao wanatangamana mara kwa mara na washiriki

### *Je, ni kwa kiwango gani mwezeshaji anapaswa kuhusishwa katika shughuli za uchoraji?*

Ikiwa inawezekana, uamuzi wa kuwa na ushiriki mkubwa au mdogo kwa mwezeshaji wa kikundi wakati wa zoezi hilo unapaswa kuridhiwa na washiriki, kwa kuzingatia uwezo wao na nia ya kufanya kazi kwa kujitegemea. Baadhi ya washiriki huenda wakahisi sawa zaidi kuandaa mchoro wakijisimamia, ilhali katika vikundi vingine, huenda wanakikundi wakahitaji usaidizi wa mwezeshaji. Washiriki huenda wakakasimisha mwezeshaji kuchora na kuandika. Katika hali hii, viwango vya ujuzi wa kusoma na kuandika vinakosa umuhimu na hivyo washirika wanaweza kulenga shabaha kwenye zoezi. Kabla ya kuwasilisha matokeo ya kila mchoro wa uhusiano katika kikundi cha pamoja, mwezeshaji wa kikundi anapaswa kuwauliza wanakikundi iwapo yeyote anajihisi kuwa tayari kuwasilisha mchoro wao kwa washiriki wengine. Sio kila mtu anakuwa mwepesi wa kuzungumza mbele ya hadhara, kwa hivyo wawezeshaji wa kikundi wanaweza kufanya wasilisho ikiwa wanakikundi wanasita. Mwezeshaji wa kikundi anaweza kukaribisha mawasilisho



*Washiriki wa mafunzo ya FMNR wakati wa kipindi cha mchoro wa uhusiano. © World Vision Ethiopia*

***Nini kinapaswa kuzingatiwa wakati wa kuchagua muundo wa shughuli ya uchoraji?***

Kwa kutegemea usuli wa washiriki (k.m., viwango vyao vya uwezo wa kusoma na kuandika, mapendeleo na mahitaji) na malengo ya somo yanayoazimiwa kutimizwa, wawezeshaji wanaweza kuchagua baina ya muundo sanifu au usio-sanifu sana. Katika muundo ambao si sanifu, washiriki wanaweza kuendelea kulingana na hatua zilizoelezwa katika sehemu iliyoko hapo juu. Wanaandika vipengele vyote ambavyo wanahusisha na uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili. Katika muundo sanifu zaidi, wawezeshaji huamua vijimada awali (k.m., kiuchumi, kijamii, kiufundi) ambavyo vinaweza kuwasilishwa mwanzoni au wakati wa shughuli ya uchoraji. Baadaye washiriki wanaombwa kulenga vipengele kutokana na vijimada hivi.

## Vyanzo vya taarifa ya ziada:

- Fischer, G., Wittich, S., & Fründt, S. (2019). Gender analysis in farming systems and action research; A training Manual. International Institute of Tropical Agriculture. https://cgspace.cgiar.org/handle/10568/100149
- Hall, R., Brent, Z., Franco, J., Isaacs, M., & Shergo, T. (n.d.); A Toolkit for Participatory Action Research. https://www.tni.org/files/publication-downloads/a_toolkit_for_participatory_action_research.pdf

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 7: Somo la 2.1 muhtasari*

| **Muhtasari** | **Michoro ya uhusiano ya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili** |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 75 |
| **Malengo ya Somo** | • Washiriki wametafakari kuhusu vipengele na vichocheo vilivyobainishwa vya uharibifu wa mazingira katika miktadha yao<br>• wametafakari kuhusu vipengele na vichocheo vilivyobainishwa vya ukataji miti katika familia na jamii yao<br>• wametafakari kuhusu mikakati na mbinu za usimamizi wa mali asili katika familia na jamii yao |
| **Mada** | ◊ Mchoro wa uhusiano na uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili.<br>◊ Mchoro wa uhusiano kama nyenzo ya tafakari shirikishi katika kikundi<br>◊ Uhusiano baina ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili. |
| **Maandalizi** | ○ Andaa chumba kwa ajili ya kazi ya vikundi (meza 5 hadi 6 na viti, chati na Kalamu za Kuandikia Ubaoni za rangi tofauti)<br>○ Andaa mawasilisho ya PowerPoint au bango lenye maagizo kwa kazi ya vikundi kwa kutumia mchoro wa uhusiano<br>○ Andaa kielelezo / mfano wa mchoro wa uhusiano (tazama Nyongeza ya 1) |

| | | |
|---|---|---|
| **Nyenzo** | ➢ Chati (moja kwa kikundi cha washiriki 4 hadi 6)<br>➢ Kalamu za Kuandikia Ubaoni (za rangi tofauti)<br>➢ Wasilisho la PowerPoint au bango<br>➢ Kielelezo cha mchoro wa uhusiano<br>➢ Matini zenye maagizo |
| **Mbinu** | ❖ Mawasilisho<br>❖ Kazi ya vikundi<br>❖ Mdahalo wa pamoja |
| **Maelekezo** | ○ Utekelezaji wa somo hili huenda ukahitaji uhusisho wa zaidi ya mwezeshaji mmoja, hasa kusaidia katika kazi ya vikundi.<br>○ Wawezeshaji wanapaswa kuhimiza ushiriki tendaji wa washiriki wote wa warsha katika shughuli hii |

### Hatua na maagizo

**Hatua ya 1:** Ili kuelewa FMNR na kwa nini itumike, ni muhimu kwanza kutafakari kuhusu muktadha wa ndani na kuzingatia masuala ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na matumizi ya mali asili. Eleza kwamba somo hili linatanguliza nyenzo ya tafakari shirikishi katika kikundi ili kusaidia kutambua vipengele muhimu vinavyohusiana na dhana husika: mchoro wa uhusiano.

**Hatua ya 2:** Tanguliza muundo wa somo. Katika sehemu ya kwanza, kikundi kitapokezwa ufahamu wa jumla wa michoro ya uhusiano kama nyenzo ya kushiriki; katika sehemu ya pili, washiriki watagawanywa katika vikundi 5 hadi 6 ili kuchora michoro ya uhusiano, pamoja na kujadili na kutambua vipengele muhimu na vichocheo vinavyohusika na dhana tatu zinazozingatiwa. Mwisho, eleza kwamba zoezi hili litafuatiwa na majadiliano ya pamoja kuhusu matokeo ya kazi ya vikundi, tajriba na mafunzo yanayopatikana kutokana na zoezi hili.

**Hatua ya 3:** Wasilisha mchoro wa uhusiano na uwaeleze washiriki kuhusu vipengele vyake vikuu. Unaweza kutumia taarifa za kiusuli iliyotolewa katika sehemu iliyotangulia na utumie kielelezo cha mchoro wa uhusiano kutoa mfano na marejeleo (tazama Nyongeza ya 1) Jibu maswali yafuatayo kwa niaba ya washiriki:

- Je, upeo wa mchoro wa uhusiano katika warsha hii ni upi?
- Je, mchoro wa uhusiano una vipengele gani?
- e, mchoro wa uhusiano unaundwa vipi?

Unaweza pia kutumia chati kueleza maagizo ya jumla. Uliza ikiwa washiriki wako na maswali au maoni.

**Hatua ya 4:** Baada ya wasilisho hili, wagawe washiriki katika vikundi kulingana na mapendekezo yaliyotolewa katika sehemu ya "'Usuli wa kinadharia'. Elekeza kila kikundi mezani kwa kazi ya vikundi; kila mwezeshaji anapaswa kujiunga na kikundi ikiwa itahitajika.
Gawa matini zenye maagizo na upitie kila hatua katika vikundi hivi vidogo.

**Hatua ya 5:** Vikundi vinazamia shughuli ya uchoraji. Baada ya takriban dakika 20, omba vikundi kubainisha vipengele na vichocheo muhimu vya uharibifu wa kimazingira na ukataji wa miti ambavyo ni maalum kwa muktadha wao, pamoja na mikakati na mbinu za usimamizi wa mali asili ambazo zinaweza kushughulikia vipengele hivi. Kamilisha zoezi la uchoraji baada ya takriban dakika 30.

**Hatua ya 6:** Baada ya kukamilisha zoezi, omba kikundi kitundike michoro yao ya uhusiano katika sehemu ya ukuta uliotengwa chumbani. Waalike washiriki kutazama kile ambacho vikundi vingine vimeandaa. Baada ya dakika chache, waombe warejee

Kwenye kikundi cha pamoja - huku viti vikiwa vimepangwa kwa umbo la nusu duara ili waweze kuona mabango tofauti.

**Hatua ya 7:** Anza majadiliano ya pamoja. Omba mwanakikundi mmoja kutoka kila kikundi kuwasilisha kwa kifupi vipengele ambavyo vimeibuka katika mchoro wao wa uhusiano. Wakati wa kila wasilisho, karibisha maswali na maoni kutoka kwa washiriki wengine.

**Hatua ya 8:** Baada ya michoro yote ya uhusiano kuwasilishwa na kujadiliwa, anzisha majadiliano kuhusu nyenzo hiyo. Waulize washiriki kuhusu tajriba zao wakati wa shughuli ya uchoraji. Kuhusu mchakato: Nini kilienda vizuri? Ni changamoto zipi walipitia? Kuhusu nyenzo: Walipendezwa kwa kiwango gani na nyenzo hiyo? Nini kiliwapendeza na nini hakikuwapendeza kuhusu nyenzo hiyo?

**Hatua ya 9:** Hitimisha somo kwa kueleza kuwa mchoro wa uhusiano unaweka msingi kwa somo linalofuata la warsha na kwa hivyo linasaidia utambuzi wa kiingilio kwa FMNR katika muktadha mahususi. Tambua na uwashukuru washiriki kwa michango yao na kutoa maoni yao kabla ya kuendelea kwenye somo linalofuata.

## Maagizo kwa mwendeshaji:

- Washiriki wanaweza kuunganika vyema na wasilisho la mchoro wa uhusiano kwenye karatasi kuliko onyesho la PowerPoint. Hivyo basi, inapendekezwa Kuwasilisha mfano wa mchoro wa uhusiano kwenye bango (k.m., kutokana na uchunguzi kifani au mafunzo ya awali) na kuuweka juu ya meza kubwa. Waalike washiriki kusimama kando ya meza hiyo huku ukieleza hatua 1 hadi 3
- Katika hatua ya 8, majadiliano kuhusu mchoro wa uhusiano yanapaswa kuakisi tajriba kutokana na nyenzo badala ya maudhui ya zoezi.
- Kama mwendeshaji, inapendekezwa kurekodi na kuhifadhi michoro ya uhusiano na mawasilisho yaliyozalishwa wakati wa kazi ya vikundi kwa ajili ya usimamizi wa ufahamu na mafunzo ya baadaye.
- Mfano wa mwongozo wa hatua kwa hatua unaweza kupatikana katika ukurasa wa 50 katika International Institute of Tropical Agriculture's Gender analysis in farming systems and action research: A training manual.

## Somo la 2.2: Masuala ya msingi kuhusu uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili

### Usuli wa kinadharia:

Mifumo ya ikolojia na mali asili huweka msingi kwa maisha ya binadamu na viumbe hai wote kwa kupeana maji, hewa na rasilimali za ardhi. Mifumo ya ikolojia kama vile misitu hutoa huduma anuwai za mifumo ya ikolojia ikiwemo uundaji wa udongo, mzunguko wa virutubishi, udhibiti wa tabianchi na maji, usafishaji wa maji, uchavushaji, chakula, maji safi na kuni, burudani ya asili, na elimu. Mifumo ya ikolojia ya misitu ambayo ni bora na yenye afya hulinda vyanzo vya maji na kupunguza hatari za majanga kwa binadamu, kama vile maporomoko ya ardhi na mafuriko. Ulimwenguni, watu bilioni 1.6 hutegemea misitu kwa riziki yao (UNEP n.d.). Kwa hivyo, usimamizi endelevu na matumizi yenye usawa ya mali asili ni muhimu kwa maendeleo endelevu.

### Uharibifu wa kimazingira na ukataji wa miti

Baada ya michoro yote ya uhusiano kuwasilishwa na kujadiliwa, anzisha majadiliano kuhusu nyenzo hiyo. Waulize washiriki kuhusu tajriba zao wakati wa shughuli ya uchoraji. Kuhusu mchakato: Nini kilienda vizuri? Ni changamoto zipi walipitia? Kuhusu nyenzo: Walipendezwa kwa kiwango gani na nyenzo hiyo? Nini kiliwapendeza na nini hakikuwapendeza kuhusu nyenzo hiyo?

Uharibifu wa kimazingira unajumuisha kupungua kwa rasilimali muhimu za asilia, ikiwemo maji, hewa, udongo, mimea, wanyama, na vipengele vingine vya mazingira, uharibifu wa mifumo ya ikolojia na uchafuzi wa mazingira. Kutokana na uharibifu, mifumo ya ikolojia haiwezi tena kutoa bidhaa na huduma kwa ufanisi kwa watu na kwa dunia. Kwa hakika, uharibifu wa ardhi unaelezwa na ni upotezaji wa muda mrefu wa kikaboni ya udongo, upunguzaji au upotezaji wa uzalishaji wa kibiolojia, uadilifu wa kiikolojia au thamani kwa binadamu (IUCN, 2015). Ulimwenguni, takriban asilimia 25% ya eneo zima la dunia limeharibiwa (GEF, n.d), na hivyo kufanya uharibifu wa ardhi kuwa tatizo mojawapo sugu la kimazingira na linaloibua changamoto kubwa kwa uhifadhi wa uanuwai wa viumbe, maendeleo endelevu, na ukabilianaji na urekebishaji wa mabadiliko ya tabianchi. Wakati uharibifu wa ardhi unapotokea katika maeneo kame, hii hujulikana kama kuenea kwa jangwa.

Uharibifu wa ardhi unatokana na mabadiliko anuwai ya kibiolojia na kimaumbile yanayohusiana, jambo ambalo tunaweza kuligawa katika aina tatu kuu zinazohusiana na (1) udongo, (2) uoto na misitu, na (3) rasilimali za maji, ambazo zinaweza kugawika zaidi kulingana na aina ya mchakato wa uharibifu. Aina hizi zinajumuisha aina ndogo za michakato ya uharibifu, ikiwemo mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa udongo kibiolojia, kikemikali na kimaumbile, uharibifu wa uoto na misitu, ukataji wa miti, pamoja na uharibifu wa rasilimali ya maji (Tazama Nyongeza ya 2). Uharibifu wa ardhi unasababishwa na michakato inayosababishwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na binadamu, ikiwemo mabadiliko ya tabianchi kutokana na shughuli za binadamu. Usimamizi usio endelevu wa ardhi, kwa mfano katika sekta ya kilimo (k.m., kupitia ulimaji wa kawaida, ufugaji wa mifugo wengi) pamoja na mabadiliko katika matumizi ya ardhi (kupitia kwa ukataji wa mimea na misitu na ubadilishaji wa misitu na vinamasi) ni miongoni mwa visababishi vya dhati vinavyochangia uharibifu (Olsson et al., 2019). Masuala haya yanazidishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Isitoshe, ukosefu wa ulinzi wa umiliki wa ardhi na sera dhaifu za kimazingira na masharti ya uhifadhi wa mali asili yanachangia mtindo huu hasi katika hali ya ardhi. Kwa hivyo, uharibifu wa radhi unaathiri vibaya vipengele mbalimbali vya maisha ya binadamu, kukiwa na athari za kijamii, kisisasa, kitamaduni na kiuchumi, na kusababisha athari kubwa kwa vikundi vya kijamii na mifumo ya uchumaji riziki inayotegemea mali asili. (Olsson et al., 2019).

Watu, familia na jamii ambazo zinategemea mali asili moja kwa moja kwa maisha yao, mapato na usalama wa chakula (ikiwemo wanawake, vijana, watu walio na ulemavu na vikundi vya jamii za kiasili zenye uwezo mdogo wa kubadilika) zipo katika hatari zaidi kutokana na uharibifu wa kimazingira au ardhi. Uharibifu wa ardhi hupunguza uwezo wa uzalishaji wa ardhi na kuongeza kazi ya usimamizi wa ardhi, ambayo katika baadhi ya maeneo huathiri wanawake kwa kiasi kikubwa zaidi. Isitoshe, ukataji wa miti unasababisha upungufu katika ufikiaji wa kuni, wana-jumuiya wanalazimika kwenda mbali, na hivyo kuongeza mzigo wa majukumu na kuzidisha muda unaotumika katika kukusanya kuni. Vivyo hivyo, uharibifu wa ardhi na ukataji wa miti unaweza kuwa na athari kubwa kwa mifu-mo ya maji, kuathiri ubora na wingi wa maji na kusababisha athari hasi kwa watu na riziki zao. Mifano ya hali hizi inajumuisha kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira na mchanga katika vijito na mito pamoja na kukauka kwa vyanzo vya maji na kupunguza viwango vya maji yaliyoko chini ya ardhi.

Uharibifu wa kimazingira kwa hivyo unaweza kuleta au kuzidisha ushindani kwa rasilimali finyu kupitia kwa vitisho vingi vinavyohusiana, hali ambayo inaathiri kwa njia hasi usalama wa chakula, umasikini, migogoro na uhamaji miongoni mwa watu na jamii za mashambani.

**Usimamizi wa mali asili**

Kwa watu na jamii zinazoishi katika maeneo yaliyoharibi-wa - ambao riziki yao, usalama wa chakula na mapato moja kwa moja yanategemea mali asili – kuepuka, kupunguza au kurekebisha uharibifu wa kimazingira ni jambo muhimu sana. Matumizi endelevu ya mali asili (kama vile maji, hewa, ardhi, misitu, samaki, na mimea na wanyama wa mwituni) hupungu-za na kuzuia uharibifu zaidi na kuimarisha huduma za mifumo ya ikolojia, ambazo ni muhimu kwa maisha bora ya binadamu. Usimamizi endelevu wa mali asili kwa wakati huo huo huleta manufaa ya pamoja kama vile urekebishaji na ukabilianaji wa mabadiliko ya tabianchi.

Usimamizi endelevu wa mali asili unahusisha mbinu mbalim-bali za urejesho/urejeshaji na mielekeo ya usimamizi wa mandhari. Hii inajumuisha miundomsingi ya uhifadhi wa udongo na maji (k.m., matuta, mitaro, mabwawa ya udhibiti, mabwawa ya mchanga au boma la kukingia mto), upandaji wa nyongeza pamoja na mielekeo kama vile usimamizi ende-levu wa matumizi ya ardhi.



## Vyanzo vya taarifa ya ziada:

- Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC). (2019). 'Land degradation'. https://www.ipcc.ch/site/assets/uploads/sites/4/2022/11/SRCCL_Chapter_4.pdf
- Muller, A., Lindell, C., de Villier, I., Garrett, J., Ondere, L.; Zoueini, R., Kelly, R., McKenzie, S., Banu Immanuel, S., Jabeen, S., & Yamada Morovic, Y. (2023). Regreening Communities Handbook. World Vision International. https://www.wvi.org/publications/field-guide/climate-change/project-model-handbook-regreening-communities
- World Vision and GIZ. (2021). Forestmaker – Training on FMNR. (Video, 14:34). https://youtu.be/K7aOkCs1PuE?feature=shared

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 8: Somo la 2.2 muhtasari*

| Muhtasari | Masuala ya msingi kuhusu uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 30 |
| **Malengo ya Somos** | ➢ Washiriki<br>➢ watafahamu vipengele na dhana muhimu za uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili<br>➢ watajua viungo muhimu baina ya dhana hizi tatu<br>➢ watafahamu athari za uharibifu wa kimazingira na ukataji wa miti kwa riziki |
| **Mada** | ◊ Dhana ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili.<br>◊ Uhusiano baina ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili |
| **Maandalizi** | ○ Andaa wasilisho la PowerPoint au bango lenye misingi ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili<br>○ Andaa karatasi za chati, kadi na Kalamu za Kuandikia Ubaoni |
| **Nyenzo** | • Chati<br>• Wasilisho la PowerPoint au bango<br>• Kadi<br>• Kalamu za Kuandikia Ubaoni |
| **Mbinu** | ➢ Mawasilisho<br>➢ Mdahalo wa pamoja |

**Hatua na maagizo**

**Hatua ya 1:** Anza somo kwa kurejelea dhana tatu zilizoshughulikiwa katika shughuli iliyotangulia, mchoro wa uhusiano. Eleza kwamba somo hili linatanguliza misingi ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili.

**Hatua ya 2:** Wasilisha vipengele muhimu vya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili. Unaweza kutumua taarifa za kiusuli zilizotolewa katika sehemu iliyotangulia na kuandika maneno muhimu na maelezo kwenye chati ili kusaidia katika ufafanuzi.

**Hatua ya 3:** Baadaye, rejelea michoro ya uhusiano iliyoandaliwa na washiriki kueleza na kusisitiza jinsi imedhihirisha uhusiano baina ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili. Waulize washiriki iwapo wana maswali yoyote

**Hatua ya 4**: Baada ya wasilisho hili, gawa kadi tupu kwa washiriki na uwaulize swali lifuatalo: "Je, nini madhara ya uharibifu wa kimazingira au uharibifu wa ardhi na ukataji wa miti kwa riziki zenu?" Waombe washiriki waandike maneno machache kujibu swali hili kutokana na tajriba zao kwenye kadi ulizowapa. Zoezi hili linapaswa kuchukua takriban dakika 5 hadi 7.
Wakishakamilisha, kila mshiriki anapaswa kutundika kadi yake kwenye chati ambayo umeandaa kuhusu swali hili la riziki.

**Hatua ya 5:** Baada ya kazi zote kukusanywa na kutundikwa, katika kikao cha pamoja, mnaweza kupitia na kuchakata maoni ya washiriki ili kuangazia athari za moja kwa moja na zisizokuwa za moja kwa moja za uharibifu wa kimazingira na ukataji wa miti kwa riziki za watu.

**Hatua ya 6:** Hitimisha kwa kueleza haja, umuhimu, na dharura ya mikakati ya usimamizi wa mali asili ili kushughulikia athari hasi kwa riziki na kukabili, kuepuka na/au kurekebisha uharibifu wa ardhi.

## Somo la 2.3: Utangulizi kwa urejesho wa msitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii

### Usuli wa kinadharia

Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii ni mwelekeo wa kurejesha misitu na mandhari yaliyoharibiwa na kuboresha ustawi wa binadamu ambao unahusisha jamii za ndani kiutendaji katika kupanga, kutekeleza, na kusimamia shughuli za urejesho. Mbinu za urejesho wa misitu na mandhari zimethibitishwa kuwa na manufaa mengi katika kuhifadhi uanuwai wa viumbe, kusaidia upataji endelevu wa riziki na chakula cha kutosha, na kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi. Hii inajumuisha kutenga kaboni na kupunguza utoaji wa gesi chafuzi, kuboresha ustahimilivu wa mandhari na kupunguza hatari za majanga.

**Manufaa ya Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii**

Urejesho wa misitu na mandhari unaojikita katika jamii husaidia kurejesha miti pamoja na kuboresha mandhari kwa kurejesha huduma za mfumo wa ikolojia kama vile rutuba ya udongo, uchujaji wa maji, uanuwai wa viumbe na udhibiti wa hali ya hewa katika sehemu maalum, ambayo hatimaye hupunguza hatari ya matukio mabaya ya hali ya hewa. Kuboresha na kulinda uoto huleta ongezeko la
chembechembe za asili katika udongo, uthabiti wa nitrojeni na udongo, uhifadhi wa mimea na viumbe, pamoja na uzalishaji wa mazao ya misitu ya mbao na yasiyo ya mbao.
Kwa hivyo, urejesho wa misitu na mandhari unaojikita katika jamii uko na uwezekano wa kutoa manufaa ya kurekebisha na kudhibiti tabia nchi ya eneo pana. Urejesho wa misitu na miti unaweza kuchangia uthabiti wa tabianchi ya ndani kwa kuwa unaweza kuchangia mvua kupitia kwa mchakato wa uhamishaji wa maji kutoka kwa ardhi hadi angani, kupunguza athari za joto, na kutoa makazi kwa mimea na viumbe anuwai na kutoa nafasi za kazi kwa wenyeji (Garrett, 2022). Isitose, wingi wa uoto pia hutenga na kuhifadhi kiasi kikubwa cha kaboni kutoka angani, na hivyo kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.
Manufaa ya urejesho wa kimazingira kwa hivyo hupiga hatua zaidi ya kurejesha mfumo wa ikolojia ulioharibiwa; unaweza kuibua matokeo chanya ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Udongo ulio thabiti na uzalishao zaidi, uoto, njia za maji na maeneo ya pwani na majini hunufaisha familia na jamii ambazo zinategemea mazingira kwa mapato, chakula, dawa na upunguzaji wa hatari.

### Vyanzo vya taarifa ya ziada:

- International Union for Conservation of Nature (IUCN) (n.d.). 'Forest landscape restoration'. https://www.iucn.org/our-work/topic/forests/forest-landscape-restoration
- Mwangi, E.; & Evans, M. (2018). Communities restoring landscapes: Stories of resilience and success. Center for International Forestry Research. https://www.cifor.org/knowledge/publication/6980/

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 9: Somo la 2.3 muhtasari*

| **Muhtasari** | **Utangulizi kwa Urejesho wa mandhari ya msitu (FLR) iliyo katika jamii** |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 30 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki<br>➢ watapata uelewa wa kimsingi wa dhana ya urejesho wa mandhari na misitu unaojikita katika jamii<br>➢ wanafahamu athari chanya za kimazingira za miti na uoto mwingine kuhusu hali ya hewa katika sehemu maalum, muundo na ubora wa udongo, na mifumo ya maji |
| **Mada** | ◊ dhana ya urejesho wa mandhari unaojikita katika jamii<br>◊ Manufaa ya kimazingira ya uoto kwa hewa katika sehemu maalum, muundo na ubora wa udongo., na usimamizi wa maji. |
| **Maandalizi** | ▪ Andaa onyesho la PowerPoint au bango lenye taarifa muhimu kuhusu urejesho wa misitu na mandhari unaojikita katika jamii<br>▪ Andaa karatasi za chati na Kalamu za Kuandikia Ubaoni |
| **Nyenzo** | ❖ Wasilisho la PowerPoint au bango<br>❖ Chati<br>❖ Kalamu za Kuandikia Ubaoni |
| **Mbinu** | O Mawasilisho<br>O Mdahalo wa pamoja |

**Hatua na maagizo**

**Hatua ya 1:** Watangulize washiriki kwa somo la mwisho la kitengo hiki cha mafunzo. Eleza kwamba watajifunza kuhusu urejesho wa misitu na mandhari unaojikita katika jamii na manufaa yake anuwai katika kudhibiti uharibifu wa kimazingira na ukataji wa miti.

**Hatua ya 2:** Kabla ya wasilisho, wahimize washiriki kutafakari kuhusu maana ya urejesho wa misitu na mandhari unaojikita katika jamii na vipengele vyake, na uwaombe washiriki maoni yao na wachangie. Wezesha majadiliano na urekodi michango ya washiriki kwenye chati.

**Hatua ya 3:** Baadaye, rejelea michoro ya uhusiano iliyoandaliwa na washiriki kueleza na kusisitiza jinsi imedhihirisha uhusiano baina ya uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili. Waulize washiriki iwapo wana maswali yoyote

**Hatua ya 4**: Baada ya wasilisho hili, gawa kadi tupu kwa washiriki na uwaulize swali lifuatalo: "Je, nini madhara ya uharibifu wa kimazingira au uharibifu wa ardhi na ukataji wa miti kwa riziki zenu?" Waombe washiriki waandike maneno machache kujibu swali hili kutokana na tajriba zao kwenye kadi ulizowapa. Zoezi hili linapaswa kuchukua takriban dakika 5 hadi 7. Wakishakamilisha, kila mshiriki anapaswa kutundika kadi yake kwenye chati ambayo umeandaa kuhusu swali hili la riziki.

**Hatua ya 5:** Wakaribishe washiriki waulize maswali au kutoa maoni kuhusu mada ambazo zimeshughulikiwa katika somo hili na/au kitengo cha ujifunzaji.

**Hatua ya 6:** Baada ya kushughulikia maswali/maoni. Washukuru watu kwa kushiriki kikamilifu na ufunge kipindi cha mwisho cha kitengo hiki cha ujifunzaji.

## Maagizo kwa mwendeshaji:

- Katika sehemu ya 4, inapendekezwa uwaombe washiriki watafakari mwingiliano baina ya somo lililotangulia (Somo 2.2) na somo la sasa.
- Ni muhimu kuhakikisha ushiriki sawa miongoni mwa washiriki wote, ukihakikisha kwamba kila mmoja ana fursa sawa ya kuchangia na kushiriki.

## Kitengo 3 cha ujifunzaji: Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR)

Kitengo cha tatu cha ujifunzaji kinawakilisha msingi wa FMNR, mbinu na upeo wake. Kinajumuisha masomo manne ambayo yanawapa washiriki uelewa wa kina wa mwelekeo huu. Katika somo la kwanza, washiriki watajifunza kuhusu dhana ya FMNR na vipengele vyake vya jumla, na kufuatiwa na maelezo ya FMNR kama mbinu ya kiufundi katika somo la pili. Somo la tatu linalenga kutanguliza mchakato wa vipengele vya FMNR na kuzidisha FMNR kama mchakato wa vipengele vya FMNR na kuzidisha FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii. Mwisho, somo la nne linahitimisha kwa kueleza upeo wa kutumia FMNR.

***Mchoro 3 Kitengo 3 cha ujifunzaji: Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR)***

**Somo la 3.1: Utangulizi wa FMNR**
Katika somo hili, tutatanguliza dhana ya FMNR kupitia kwa "gurudumu la maswali". Hii inajumuisha uwasilishaji na majadiliano ya "Nini? Kwa nini? Nani? Wapi? Na Vipi? Kipindi hiki kitawaruhusu washiriki kutafakari na kujadili kila mojawapo ya maswali haya matano, huku wawezeshaji wa warsha wakichangia vipengele muhimu kwa kila swali. Hii pia itajumuisha wasilisho la manufaa makubwa ya riziki ambazo FMNR inaweza kusaidia.

**Somo la 3.2: FMNR kama mbinu ya kiufundi**
Somo hili litaangazia vipengele vya mbinu ya FMNR (chagua, pogoa, simamia, tumia)

**Somo la 3.3: FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii**

Somo hili linatanguliza vipengele vya mchakato wa FMNR (unganisha, panga, wezesha) na linalenga kuwaelewesha washiriki kwamba FMNR inahitaji uanzishaji wa mipangilio fulani ya jamii na taasisi/kanuni (k.m., matumizi ya miti na rasilimali nyingine za asili).

**Somo la 3.4: Upeo wa kutumia FMNR**
Somo hili linatanguliza aina tofauti za mandhari na azma ambapo FMNR inaweza kutumiwa (k.m., shamba, ardhi ya malisho, misitu).

**Somo la 3.1: Utangulizi wa FMNR**

## Usuli wa kinadharia

Somo la 3.1 linatanguliza dhana ya FMNR pamoja na gurudumu la maswali matano. Maswali haya ni:

### 1. FMNR ni nini?

Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR) ni mwelekeo wa gharama ya chini, unaojikita kwa ushahidi, unaotumiwa kushughulikia ukataji miti na uharibifu wa mandhari kupitia urejesho na uboreshaji wa mashamba, misitu na ardhi ya malisho. FMNR sio upandaji wa miti. Kinyume chake, FMNR hujikita katika kuotesha upya na usimamizi wa miti na vichaka vilivyopo kutoka kwa visiki vya miti, mifumo ya mizizi inayochipua na miche iliyopo. FMNR inaweza kutumiwa popote palipo na kisiki cha mti ambacho ni hai chenye uwezo wa kuchipua upya au kukua kutokana na mbegu zilizoota.

FMNR ni mbinu ya kiufundi na ni mwelekeo wa maendeleo ya jamii unaohamasisha na kuwezesha jamii za ndani kuzalisha upya aina tofauti za mandhari.

### 2. Nani anatekeleza mwelekeo wa FMNR?

Kwa jumla, watu ambao hutekeleza FMNR ni wale ambao binafsi wanatumia au kutegemea rasilimali za miti. Hii inajumuisha wakulima, wafugaji, wanajamii, na hasa wanawake na watoto ambao huvuna bidhaa za misitu ambazo ni za mbao na zile zisizokuwa za mbao. Kwa kuwa mchakato wa FMNR ni rahisi sana, wa gharama ya chini na wenye athari kubwa, kikundi chochote au jamii ambayo inakabiliwa na matatizo kama vile ukosefu wa mbao za kutosha, mmomonyoko wa udongo, upunguaji wa miti, mazao ya chini au mapato ya chini kwa riziki zinazotegemea mali asili wanaweza kupewa mafunzo ya kutumia FMNR.

Wanajamii ambao tayari wana hamu na wanahusika katika uhifadhi na usimamizi endelevu wa miti huenda wakawa washiriki bora wa kwanza, kwa nia ya kuathiri jamii nzima baada ya muda. Vikundi vinavyowezekana ambavyo huenda vina hamu ya kuhusishwa katika vikundi vinavyolenga mwelekeo huu vinajumuisha vyama vya ushirika vya wanawake na wakulima, miungano ya ajira kwa vijana, vikundi vya kuweka akiba na kutoa mikopo, wakulima binafsi, mashirika ya kijamii na vikundi vya kidini.

### 3. FMNR inapaswa kutekelezwa lini?

FMNR inaweza kutekelezwa katika mazingira mengi tofauti kuanzia maeneo kame hadi sehemu nyevu za kitropiki. Kwa kuwa FMNR ni nafuu na huchangia masuala mengi yenye thamani, kanuni ya kimsingi ni kuzingatia kuitumia katika hali yoyote ambapo upunguaji wa miti una athari hasi kwa ustawi wa binadamu na ambapo

visiki hai vya miti au mbegu zilizojiatika zinapatikana katika mandhari.

Vifuatavyo ni viashiria ambavyo huenda vikawa muhimu katika kuelewa lini FMNR inapaswa kuzingatiwa:

- dalili za kupungua kwa mapato ya watu wanaotegemea mali asili
- mazao ya chini kutokana na mmomonyoko wa udongo, kiangazi, mafuriko au uharibifu wa upepeo, kupungua kwa rutuba ya udongo



*Kipindi cha utendaji nyanjani wakati wa mafunzo ya FMNR.*
*© World Vision Ethiopia*

- upunguaji wa miti wenye athari hasi kwa mazao ya chakula na uzalishaji wa mifugo, na ongezeko la upepo mkali, kiangazi, mafuriko, viwango vya joto na hatari zingine
- kutoweka kwa viwango vya juu vya uanuwai wa kimazingira na hamu ya jamii kufanya urejeshoupungufu wa kuni na mbao za kujengea
- ardhi yenye uwezo wa kuzalisha kutoweka kutokana na mmomonyoko wa udongo na hali ya hewa inayozidi kuwa mbaya
- mabadiliko baina ya mvua nyingi kupita kiasi na mvua isiyotosha
- wanajamii wanalazimika kuhama kutafuta kazi kutokana na kupungua kwa mazao ya chakula na faida za mashamba

### 4. FMNR inapaswa kutekelezwa vipi?

Mchakato wa FMNR unajumuisha mbinu ya kiufundi na mchakato wa maendeleo ya kijamii. Mbinu ya kiufundi ni sahili sana na inatumika kukuza na kusimamia miti na vichaka vilivyopo na kuzalisha upya mandhari husika. Inajikita katika vipengele vinne: kuteua, kupogoa, kusimamia, kutumia. Vipengele hivi vimejadiliwa kwa kina zaidi katika somo la 3.2 ambalo linafuata.

Kama mchakato wa maendeleo ya jamii, utekelezaji wa FMNR wenye ufanisi unahitaji ushiriki tendaji na uhusishwaji wa wanajamii. Vipengele vitatu vimebainishwa kuelekeza mchakato wa FMNR: unganisha, panga, wezesha. Vipengele hivi vimeelezwa katika somo la 3.3.

Isitoshe, utekelezaji wa FMNR kwa pamoja na mielekeo mingine ya usimamizi wa mali asili unaweza kusaidia kuleta mazingira yanayohitajika kuongeza kasi ya ukuaji upya wa miti na mandhari. Ujumuishaji wa mbinu jalizi za usimamizi wa mali asili unaweza kuhusisha kupanda miti ya ziada au kuatika mbegu kwenye maeneo wazi au tupu ambayo hayana vitu kama vile visiki hai na/au mbegu za mwituni. Mbinu hii pia huitwa upandaji wa kuzidisha. Mfano mwingine ni uwekaji wa majengo madogo ya kukusanya maji ya mvua na miundomsingi ya uhifadhi wa udongo na maji (k.m., matuta, mitaro, mabwawa ya udhibiti, mabwawa ya mchanga au boma la kukingia mto)

### 5. Kwa nini FMNR ni muhimu kwa maendeleo ya riziki?

Matokeo ya FMNR yanasaidia mazingira pamoja na jamii ambazo zinategemea mazingira hayo kwa maisha yao. FMNR husaidia kuweka riziki inayowezekana na ambayo ni endelevu na inayohakikishia vizazi vijavyo maisha ya baadaye. Husaidia kuleta urejesho wa uzalishaji wa mandhari na hutoa fursa ya chaguzi anuwai za kujikimu. Huchangia katika uzalishaji endelevu wa bidhaa za miti ambazo zinaweza kutumia kuzalisha mapato, kama vile kuni, matunda, dawa za kiasili, chakula cha mifugo au mbao. FMNR ina athari chanya kwa usalama wa chakula kwa kuboresha uzalishaji wa ardhi ambayo inaweza kutumiwa kukuza mazao na kulisha mifugo. Zaidi ya hayo, shughuli za ziada za kimaendeleo zinazofungamana na miti, kama vile ufugaji wa nyuki, zinaweza kuimarisha matumizi ya FMNR na uendelevu wake kwa kuongeza umuhimu wake na thamani ya kiuchumi kwa familia na jamii. Kwa kuondoa ustahimilivu wa majanga kama vile kiangazi, FMNR husaidia familia kudumisha chanzo cha mapato katika vipindi vigumu (tazama Nyongeza ya 4).

**Uhusiano baina ya Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR) na Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii**

Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii ni mbinu pana inayolenga mandhari ambayo FMNR inaweza kuchangia. Urejesho wa misitu na mandhari unaojikita katika jamii unajumuisha mbinu tofauti, ikiwemo kupanda miti, kilimo cha miti, ukuaji upya wa miti na mimea, ukuaji upya uliosaidiwa na FMNR. FMNR ina uwezo mkubwa wa kuchangia urejesho wa misitu na mandhari iliyo katika jamii, hasa wakati unatekelezwa katika kiwango cha mandhari kwa watumiaji wengi wa ardhi na ardhi ya jamii, kama vile miteremko, maeneo ya kukinga misitu au katika maeneo ya kando ya mto.ya kukinga misitu au katika maeneo ya kando ya mto.

## Vyanzo vya taarifa ya ziada:

- World Vision Australia. (2018). FMNR Manual, Chapter I: Introduction to Farmer Managed Natural Regeneration. https://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2019/02/FMNR-Field-Manual-Chapter-1.pdf
- World Vision Australia. (2019). FMNR Evidence of Impact. https://www.worldvision.com.au/docs/default-source/meta-evidence-briefs/evidence-of-impact-farmer-managed-natural-regeneration.pdf
- World Vision Australia. (n.d.). Fact Sheet: How to do FMNR. http://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2014/04/FMNR-Quick-Guide.pdf
- World Vision and GIZ. (2021). Forestmaker – Training on FMNR (Video, 06:44). https://youtu.be/K7aOkCs1PuE?feature=shared
- World Vision West Africa Regional Office. (n.d.). Farmer Managed Natural Regeneration (FMNR). http://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2014/04/FMNR-Poster-English.pdf

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 10: Somo la 3.1 muhtasari*

| Muhtasari | Utangulizi wa FMNR |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 60 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki<br>❖ wameelewa kwamba FMNR inalenga ukarabati wa uoto uliopo tayari. wameelewa tofauti na uhusiano uliopo baina ya FMNR na upandaji wa miti.<br>❖ wanafahamu kwamba FMNR inahusisha mbinu ya kiufundi na mchakato wa maendeleo ya jamii<br>❖ wanafahamu manufaa ya kimazingira na uwezo wa kujikimu unaosaidiwa na FMNR<br>❖ wanajua kwamba FMNR ni kitendo endelevu ambacho kinahitaji msaada wa jamii nzima.<br>❖ wameelewa kwamba FMNR inahitaji kuunganishwa na hatua nyingine za kujikimu na mbinu za usimamizi wa mali asili |
| **Mada** | ◊ Dhana ya FMNR<br>◊ Manufaa ya riziki kutokana na FMNR |
| **Maandalizi** | O Andaa mabango mawili au matatu yenye anwani 'FMNR' (vinginevyo tupu) na uyatundike kwenye ngazi ya chati.<br>O Andaa kielelezo cha bango kwa zoezi la 'gurudumu la maswali' (tazama Nyongeza ya 5)<br>O Andaa maswali na majibu kwa zoezi la 'gurudumu la maswali' kwenye kadi (tazama taarifa ya kiusuli na Nyongeza ya 5) |
| **Nyenzo** | • Chati<br>• Kalamu za Kuandikia Ubaoni<br>• Mabango<br>• Kadi<br>• Nyenzo ya video (hiari) |
| **Mbinu** | ➢ Mawasilisho<br>➢ Usanifu shirikishi ('gurudumu la maswali')<br>➢ Majadiliano ya pamoja |

**Hatua na maagizo**

**Hatua ya 1:** Eleza kwamba somo hili linatanguliza dhana ya FMNR na vijenzi vya jumla.

**Hatua ya 2:** Wakaribishe washiriki wasimame na kukusanyika mbele ya mabango mawili au matatu yenye anwani ya 'FMNR' (vinginevyo tupu) kwenye ngazi ya chati. Waombe kutafakari na kuandika kwenye mabango tupu kile wanachohusisha na FMNR au kile ambacho wanajua kufikia sasa, iwapo wamewahi kupata tajriba ya awali. Wahimize kuandika chochote wanachofikiria kuhusu FMNR. Punde tu wanapokamilisha shughuli hii, waombe warudi kwenye viti vyao, na ushiriki na wote (kwa kusoma kwa sauti) kile ambacho kimeandikwa kwenye mabango. Washukuru washiriki na ueleze kwamba tafakari na maoni yao ni maandalizi na ni muhimu kwa zoezi linalofuata.

**Hatua ya 3:** Watangulize washiriki kwenye zoezi la 'gurudumu la maswali'. Huenda ukateua kuweka bango lenye kielelezo sakafuni katikati mwa nusu mduara wa viti au utundike kwenye ngazi ya chati, ili lionekane na washiriki wote.

**Hatua ya 4**: Eleza kwamba utatanguliza na kujadili vijenzi muhimu na vipengele vya FMNR katika gurudumu hili la maswali (tumia taarifa za kiusuli na Nyongeza ya 5).

**Hatua ya 5:** Anza kwa swali la "nini". Weka kadi yako yenye swali la 'nini' katika sehemu husika ya kielelezo na uisome kwa sauti. Waombe washiriki wapendekeze majibu na kuweka kadi za majibu ya 'nini' ambayo umeandaa. Soma kila kadi ya majibu kwa sauti inayohusiana na 'nini' kuhusu FMNR na uziweke moja baada ya nyingine katika sehemu ya 'nini'. Endelea na utaratibu sawa kwa 'nani', 'lini', 'vipi' na 'kwa nini'.

**Hatua ya 6:** Karibisha maoni na maswali kabla ya kufunga somo hili.

## Maagizo kwa mwendeshaji:

- Shughuli ya utangulizi katika Hatua ya 2 inalenga kuwahimiza washiriki kutafakari na kutathmini jinsi ufahamu wao wa sasa unahusiana na FMNR. Wakati (baada ya kukamilisha) wawezeshaji wa warsha wanasomea kikundi kizima maandishi ya washiriki kwa sauti kwenye bango, hawapaswi kutoa maoni.
- Mwanzoni mwa zoezi hili, kielelezo cha 'gurudumu la maswali' kiko tupu. Kadi zenye maswali na majibu zinaongezwa hatua kwa hatua baada ya kutangulizwa na kujadiliwa.
- ikiwa zaidi ya mtu mmoja anawezesha warsha, wawezeshaji tofauti wanaweza kuwasilisha maswali tofauti.
- Mfano wa mwongozo wa hatua kwa hatua unaweza kupatikana katika ukurasa wa 62 katika International Institute of Tropical Agriculture's Gender analysis in farming systems and action research: A training manual.


## Somo la 3.2: FMNR kama mbinu ya kiufundiwa Mkulima (FMNR)

### Usuli wa kinadharia

FMNR kama mbinu ya kiufundi ni nyumbufu sana. Inaweza kubadilika kutegemea muktadha, aina ya mti iliyochaguliwa, idadi ya miti kwa kila hekta, idadi ya mashina yaliyoteuliwa kwa kila kisiki na kiwango cha kupogoa shina. Isitoshe, mbinu ya FMNR inategemea vipaumbele vya jamii na malengo ya utekelezaji wa FMNR.

Kwa jumla, FMNR inahusisha vipengele vinne vya mbinu hii: (1) tafuta na uteue, (2) pogoa, (3) linda na utunze, na (4) kuza na utumie. Hatua hizi za kimsingi za FMNR, au mbinu, zinaweza kurekebishwa kupitia kwa majaribio ya kutambua mbinu bora zaidi ya kutimiza mahitaji ya watu kupitia kwa ardhi na kutunza miti katika miktadha yake.

*Mchoro 4 vipengele vya utendaji wa kiufundi wa FMNR. Kutoka: World Vision International.*




| TAFUTA | POGOA | LINDA | KUZA |
|---|---|---|---|
| Tambua vichaka vya kiasii vilivyo na mfumo mpana wa mizizi. | Pogoa kitaratibu matawi yote isipokuwa mashina machache yaliyo thabiti. Hii inahakikisha madini yanaelekezwa kwenye eneo moja. | Hakikisha mashina yako yamelindwa dhidi ya wanyama kadri yanavyokua. Matawi yakishamea, pogoa tena. | Endelea kufuatilia na kupogoa miti yako kadri inavyokua. |

### 1. Tafuta na uteue

Katika hatua hii ya kwanza, watekelzaji wa FMNR wanabainisha idadi ya aina za miti ya kiasili na vichaka vinavyozalishwa upya na/au kusimamiwa katika mandhari husika. Uteuzi wa aina za miti na vichaka ni sehemu muhimu ya mchakato wa FMNR kwa kuwa itaathiri pakubwa matokeo ya shughuli za FMNR.
Watekelezaji wa FMNR wanawajibikia uteuzi wa aina za miti ambayo ni muhimu sana na ya thamani zaidi kwao na jamii yao (k.m., kulima mazao, mbao na kuni, vyakula vya wanyama, ufugaji wa nyuki).
Kwa jumla, FMNR hufanya kazi na spishi za kiasili ambazo zinapatikana kiasili katika eneo lililolengwa, kuchangia uboreshaji wa uanuwai wa viumbe na uhifadhi wa ikolojia ya mazingira ya ndani huku mahitaji ya jamii yakitimizwa.
Uteuzi wa miti na vichaka hufanywa katika hatua ya pili: (1) watumiaji wa ardhi huchunguza ardhi kwa visiki vinavyochipua na/au miche na kutambua aina za miti na vichaka vilivyopo; (2) spishi za miti na mimea huteuliwa kulingana na mapendeleo ya jamii na mahitaji ya kimazingira na kijamii.

### 2. Pogoa

Baada ya spishi inayopendelewa na visiki, miti au miche kuteuliwa kwa ukuaji upya, hatua inayofuata ni upogoaji. Watekelezaji wa FMNR huondoa kwa makini mashina na matawi ya kado ya visiki na mashina ya ukuaji upya. Hii husaidia kuongeza ukuaji wake na urejeshwaji kwa kuelekeza rasilimali na virutubisho kwa mashina machache na matawi ya kando yaliyochaguliwa.

Mbinu ya upogoaji inajumuisha kanuni tatu za kimsingi za kuzingatiwa kuzuia magonjwa na uharibifu miti inayokuzwa upya. Maswali haya ni: (1) tumia vifaa vyenye makali, (2) kata ukielekea juu badala ya chini, kila inapowezekana, na (3) usipogoe mashina juu sana.

### 3. Linda na utunze

Baada ya uteuzi na kupogoa, ni muhimu kutunza na kulinda visiki na vichaka kadri vinavyokua. Watekelezaji wa FMNR husimamia upogoaji wa visiki na vichaka kwa kurejea mara kwa mara ili kupogoa mashina na matawi ya kando kwa makini. Isitoshe, visiki na vichaka vinavyosalia vinaweza kulindwa kutokana na vitisho vinavyowezekana kama vile mifugo, moto, watu na uoto shindani au magugu kupitia kwa ardhi bora ya malisho na mbinu bora za usimamizi wa mifugo.

### 4. Kuza na utumie

Miti huendelea kuchungwa na kupogolewa kadri inavyokua. Isitoshe, miti ya FMNR inaweza kutumiwa kwa sababu mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii. Watekelezaji hutumia mashina na matawi ya kando yaliyovunwa kupitia kwa mfumo wa upogoaji kwa matumizi mengine yaliyopangwa kama vile kuni, chakula kwa mifugo au matandazo. Miche ambayo inafanyiwa ukuaji upya kufuatia uvunaji wa mashina itasimamiwa ili kuongeza kasi ya ukuaji upya. Kadri miti inavyokua, watekelezaji wanaweza kunufaika kutokana na vyakula vya mwituni, dawa za kitamaduni, rangi, gundi na bidhaa nyingine za misitu ambazo sio mbao, kwa kutegemea spishi. Katika baadhi ya hali, mti wote unaweza kukatwa na kutumiwa na watekelezaji wa FMNR.



*Kipindi cha utendaji nyanjani wakati wa mafunzo ya FMNR. © World Vision Ethiopia*

**Vyanzo vya taarifa ya ziada:**

- World Vision Australia. (2018). FMNR Manual, Chapter 4: How to practice FMNR. https://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2019/03/FMNR-Field-Manual-Chapter-4_FA.pdf
- World Vision and GIZ. (2021). Forestmaker – Training on FMNR. (Video, 08:00). https://youtu.be/K7aOkCs1PuE?feature=shared
- World Vision West Africa Regional Office. (n.d.). Farmer Managed Natural Regeneration (FMNR). http://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2014/04/FMNR-Poster-English.pdf

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 11: Somo la 3.2 muhtasari*

| Muhtasari | FMNR kama mbinu ya kiufundi |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 45 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki<br>❖ wanajua vijenzi vinne vya mbinu ya FMNR<br>❖ wako na ufahamu mzuri wa kinadharia kuhusu utendaji wa kila mbinu |
| **Mada** | ◊ Vijenzi tendaji vya FMNR |
| **Maandalizi** | • Andaa wasilisho la PowerPoint au chati yenye vijenzi vinne vya mbinu ya FMNR<br>• Andaa wasilisho la PowerPoint au chati ya kueleza na kuonyesha kila kijenzi cha mbinu ya FMNR |
| **Nyenzo** | O Chati zenye karatasi<br>O Kalamu<br>O Kadi<br>O Nyenzo ya video (hiari)<br>O Wasilisho la PowerPoint (hiari) |
| **Mbinu** | ▪ Mawasilisho<br>▪ Majadiliano ya pamoja |
| **Maelekezo** | ✓ Ikiwa inawezekana, unaweza kuongezea kipindi hiki na zoezi la maonyesho ya mbinu hizi za FMNR shambani |

Hatua na maagizo

**Hatua ya 1**: Somo la awali limetoa maelezo kuhusu dhana ya FMNR. Eleza kwamba somo hili ni la kinadharia na linalenga kuashiria jinsi ya kutekeleza FMNR kupitia kwa vijenzi vinne vikuu.

**Hatua ya 2:** Tanguliza vijenzi vinne vya utekelezaji wa FMNR (tafuta,pogoa, linda, kuza). Unaweza kutumia wasilisho la Powerpoint au chati kuwasilisha mbinu hizi nne.

**Hatua ya 3:** Eleza mbinu hizi moja baada ya nyingine, ukitumia taarifa za kiusuli zilizopo hapo juu pamoja na picha na michoro kuwasaidia washiriki kuelewa vyema mwelekeo wa kiufundi. Kwa kila hatua jumuisha vidokezo tendaji kuambatana na nadharia.

**Hatua ya 4:** Mwisho, waalike washiriki katika kikao cha pamoja kuuliza maswali au maoni kuhusu mbinu hizi nne za FMNR, kabla ya kukamilisha somo na kuendelea kwenye somo linalofuata.

### Maagizo kwa mwendeshaji:


Kando na kuwasilisha vijenzi vya mbinu katika wasilisho la PowerPoint au chati, unaweza kuzingatia kuonyesha kipindi kuhusu utekelezaji wa mbinu ya FMNRkutoka kwenye video 'Forestmaker – Training on FMNR', inapatikana mtandaoni.

## Somo la 3.3: FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii

### Usuli wa kinadharia

Kando na vijenzi hivi vinne vya mbinu iliyoelezwa katika somo lililotangulia, FMNR pia ni mchakato wa uwezeshaji wa jamii ambao unabadilisha mawazo ya jamii na uhusiano wa watu na mazingira yao asili. Ili FMNR iweze kuwa mbinu endelevu iliyowekwa katika maisha ya kila siku, inahitaji mchakato wa maendeleo ya jamii Hii inajumuisha vijenzi vitatu vikuu: (1) unganisha, (2) panga na (3) wezesha.

***Mchoro 5: Vipengele vya kimsingi vya FMNR, zikiwemo mbinu nne (nusu duara ya juu) na vipengele vitatu vya mchakato (nusu duara ya chini). Kutoka: World Vision International, 2020.***




Core Components- Vijenzi muhimu
Select – Teua
Prune – Pogoa
Manage – Simamia
Utilise – Tumia
Mindset transformation – Mabadiliko ya Mawazo
Connect – Unganisha
Plan – Panga
Enable - Wezesha

### 1.Unganisha

Kwanza, wanajamii wanapaswa kuja pamoja kutalii vile mazingira yao yalikuwa hapo awali, jinsi yalivyo leo na yatakavyokuwa siku zijazo. Uelewa wa pamoja wa mazingira, pamoja na mila, uamilifu wa kimila na mienendo ya watu katika jamii, ni muhimu katika kukuza ushiriki na kutambua kile kinachohitajika ili kuboresha maisha katika jamii. Kwa hivyo, wanajamii wanapaswa (katika njia shirikishi) kuchambua, kujadili na kuunganisha sababu za msingi za ukataji miti na uharibifu wa mazingira na matokeo yanayolingana kwa jamii yao.  Baada ya kufanya uhusisho huu, FMNR inaingizwa kama suluhu inayowezekana.

### 2.Panga

Baada ya wanajamii kuamua kwamba FMNR ni mbinu faafu ya kushughulikia shauku zao za kimazingira, mpango wa utekelezaji unaweza kuundwa. Wanajamii wanashiriki katika mchakato shirikishi wa kuweka maono ili kubainisha malengo ya pamoja na kukubaliana kuhusu hatua zinazoonekana za kuendesha na kuwezesha uongezaji wa FMNR katika ardhi ya jumuiya na inayomilikiwa na watu binafsi. Mipango hii inaweza kutofautiana katika urasmi na inaweza kuendelezwa na kupigwa msasa kwa miaka mingi.

### 3.Wezesha

Shughuli za kuimarisha uwezo huwezesha wanajamii kupata maarifa ya kiufundi na ujuzi wa kukumbatia na kukuza mbinu za FMNR katika mandhari.
Hii pia inajumuisha kutambua, kutoa mafunzo na kushauri Watetezi wa FMNR wanaofanya kazi ya kuimarisha na kueneza matumizi ya FMNR katika jamii. Watetezi wa FMNR ni watu ambao wametumia na kutekeleza FMNR wenyewe kwa ufanisi na wanawafunza wengine kupitia ufahamu wao na tajriba yao katika FMNR. Katika muktadha huu, ziara miongoni mwa watekelezaji wa FMNR ni mbinu yenye nguvu katika kusaidia kuonyesha manufaa na ufanisi wa FMNR.

Aidha, usambazaji endelevu wa FMNR unahitaji kuanzishwa kwa miundo na taasisi fulani za jumuiya. Iwapo miundo hii ipo tayari, uimarishwaji wake unapaswa kuhimizwa kupitia kwa mafunzo, ushauri na mahusiano. Miundo hii inaweza kujumuisha kamati za usimamizi wa mali asili, vikundi vya kazi, mashirika na miundo sawa ya kitaasisi, kulingana na utamaduni na mahitaji ya jamii. Shughuli zingine ambazo ni muhimu zinajumuisha maendeleo na utekelezaji wa kanuni na makubaliano mengine kuhusu usimamizi endelevu wa ardhi na mali asili, maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi, na njia faafu na endelevu ya kutekeleza sheria (kama vile faini, huduma kwa jamii au mielekeo mingine iliyokubaliwa na jamii).

### Vijenzi vinavyotanda kote: Mabadiliko ya mawazo

Zaidi ya vijenzi vya maendeleo ya jamii, muhimu zaidi kwa FMNR ni mabadiliko ya mawazo ambayo hutokea kadri watu binafsi na jamii zinavyohusishwa katika mchakato wa FMNR na kukumbatia utekelezaji. Kupitia kwa mchakato wa kubadili mawazo, watu na jamii hushuhudia uhamishaji chanya katika mitazamo yao na msukumo wa kushughulikia visababishi na athari za uharibifu wa kimazingira. Matokeo yake ni mageuzi kutoka kwa kutokuwa na matumaini na kutojali hadi kuwa na matumaini na uwezeshaji kwa mustakabali wenye uendelevu na ufanisi zaidi.

**Vyanzo vya taarifa ya ziada:**

- World Vision Australia. (2018). FMNR Manual, Chapter 5: Community engagement to create sustainable FMNR practice. https://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2019/03/FMNR-Field-Manual-Chapter-5_FA.pdf
- World Vision International. (2020). FMNR – Definition and key messages.

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 12: Somo la 3.3 muhtasari*

| Muhtasari | FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 30 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki<br>❖ wanajua vijenzi vikuu vya mchakato wa FMNR<br>❖ wanafahamu miundo muhimu na taasisi zinazohitajika kuanzisha FMNR katika jamii (k.m., kamati za usimamizi wa mali asili, sheria ndogo, mipango ya matumizi ya ardhi, n.k.) |
| **Mada** | ◊ Vipengele vya mchakato wa jamii wa kutekeleza FMNR<br>◊ Miundo na taasisi kwa ushirikishwaji wa jamii katika FMNR |
| **Maandalizi** | ▪ Andaa wasilisho la PowerPoint au chati yenye vijenzi vitatu vya mchakato wa FMNR<br>▪ Andaa wasilisho la PowerPoint au chati kueleza kila kipengele cha mchakato wa FMNR |
| **Nyenzo** | O Chati zenye karatasi<br>O Kalamu za Kuandikia Ubaoni<br>O Nyenzo ya video (hiari)<br>O Wasilisho la PowerPoint (hiari) |
| **Mbinu** | ➢ Mawasilisho<br>➢ Majadiliano ya pamoja |

### Hatua na maagizo

**Hatua ya 1:** Eleza kwamba azma ya somo hili ni kuonyesha jinsi mwelekeo wa FMNR, ili uwe na uendelevu, unahitaji mchakato wa maendeleo ya jamii ambao unaweza kugawika katika vipengele vitatu vikuu.

**Hatua ya 2:** Tanguliza vipengele vitatu vya mchakato wa FMNR (unganisha, panga, wezesha). Unaweza kutumia wasilisho la Powerpoint au chati kuziwasilisha.

**Hatua ya 3:** Eleza vipengele moja kwa moja, kwa kutumia taarifa za kiusuli zilizo hapo juu pamoja na picha na michoro inayohusika, ikiwa ipo. Kwa kila hatua jumuisha vidokezo tendaji kuongezea kwa nadharia.

**Hatua ya 4:** Katika kikundi cha pamoja, waombe washiriki kuuliza maswali au kutoa maoni kuhusu vipengele vitatu vya mchakato wa , kabla ya kufunga kipindi na kuendelea kwa somo la mwisho katika kitengo hiki cha mafunzo.

**Somo la 3.4: Upeo wa kutumia FMNR**

## Usuli wa kinadharia

FMNR inaweza kutumiwa katika mazingira na mifumo tofauti ya matumizi ya ardhi kama vile ardhi ya malisho, mashamba, ardhi ya misitu, kinamasi, sehemu za miteremko au zilizoharibiwa za ardhi ya jamii.

**FMNR katika ardhi ya malisho:**

Mazingira haya huwa na miti michache, ambayo hutoa manufaa mbalimbali kama vile vyakula na kivuli kwa wanyama katika msimu wa kiangazi, huku ukiimarisha uanuwai wa viumbe. Matumizi ya FMNR huongeza uzalishaji wa nyasi kwa mifuo, jambo ambalo ni kipaumbele kwa mfumo huu wa matumizi ya ardhi. Kwa hivyo, wingi wa miti aghalabu husimamiwa ili kuepuka athari hasi kwenye nyasi na vichaka ambapo chini yake ni chanzo cha chakula kwa mifugo.

**FMNR katika mashamba:**

Mazao ya mashamba yanaweza kuzidishwa maradufu au hata kuongezwa mara tatu miti inapokuzwa pamoja na mazao mengine. Hata hivyo, hii itawezekana tu iwapo miti yenye sifa zinazofaa, kama vile miti inayosawazishisha nitrojeni, inateuliwa. Kupitia kwa FMNR, wakulima wanaweza kusaidia kudhibiti kiasi cha kivuli ambacho kitafunika mazao kwa kutumia mbinu bora za upogoaji kwa ufanisi na kudhibiti idadi ya miti inayorejeshwa.

**FMNR katika ardhi ya misitu:**

Misitu ambayo imeharibiwa kutokana na ukataji au uvunaji huenda ikawa na uanuwai mdogo wa mimea na viumbe au vichaka, na hivyo kusababisha mifumo duni ya ikolojia ya misitu. Matumizi ya mbinu za FMNR yanaweza kufaulu katika urejeshaji wa misitu iliyoharibiwa kwa kufanya urejesho wa uanuwai wa viumbe na misitu asilia. Isitoshe, misitu inayotoa manufaa endelevu, kama vile upatikanaji wa dawa za kiasili, matunda na kuni, iko na uwezekano mkubwa wa kusaidiwa na jamii inayoizingira, na hivyo kufanya utunzaji wake kuwa rahisi.

**FMNR kwa usimamizi wa maji:**

Kuongeza idadi ya miti katika maeneo muhimu kama vile kwenye miteremko ya milima na sehemu za juu za vyanzo vya maji kunaweza kusaidia kupunguza kasi ya mtiririko wa maji, na hivyo kuruhusu muda zaidi wa maji kupenyeza na kujaza hifadhi za maji ya ardhini. FMNR hivyo basi inaweza kusaidia kushughulikia masuala yanayohusiana na mmomonyoko wa udongo, kukosekana kwa ardhi thabiti, kiwango cha chumvi na kupungua kwa maji chini ya ardhi katika vyanzo au vinamasi.



**FMNR katika miteremko ya milima au ardhi iliyoharibiwa:**

Katika miktadha minigi, ardhi isiyotumika kwa kilimo iliyopo kwenye miteremko ni ya jamii kinyume na ardhi inayosimamiwa kibinafsi. Kutekeleza FMNR katika aina hii ya mazingira kwa hivyo inahitaji ushirikishwaji wa jamii kwa dhati na ushirikiano. Ikiwa jamii hazina haki za kipekee au haki kuu za kufikia ardhi, mamlaka za mitaa zinapaswa kuhusishwa ili kuhakikisha haki za kisheria za watumiaji wa jumuiya. FMNR katika ardhi ya jamii hurejesha au kuimarisha huduma mbalimbali za mifumo ya ikolojia, kama vile utoaji wa dawa za kiasili, katika chakula cha mwituni, kuni na bidhaa nyingine za msitu zisizohusiana na mbao. Pia inaboresha uchavushaji wa mazao, ulinzi wa mazao na rutuba ya udongo, pamoja na maji, mmomonyoko wa ardhi na udhibiti wa hali ya hewa.

Kama ilivyobainishwa hapo juu, utekelezaji wa mbinu za FMNR hutumika kwa aina tofauti za mazingira na unaweza kutumika kwa azma mbalimbali. Kuongeza wingi wa miti na majani kuna athari chanya kwenye rutuba ya udongo, upatikanaji wa maji, uanuwai wa mimea na viumbe na kazi nyingine za mfumo ikolojia zinazofanywa na mazingira yenye afya.

Kwa kutegemea malengo ya watekelezaji na spishi zinazorejeshwa, miti ya FMNR inaweza kusimamiwa kwa azma mbalimbali kama vile:

- kuchanganywa na mazao ya chakula na ya kuuzwa
- mipaka/ua hai
- mbao na kuni
- ufugaji wa nyuki, matunda na bidhaa za msitu zisizokuwa mbao
- chakula cha mifugo
- urejeshaji wa msitu na uhifadhi wa uanuwai wa viumbe
- uthabiti wa ardhi/udhibiti wa mmomonyoko wa udongo
- ardhi ya malisho/ardhi ya jamii
- uhifadhi wa maji.



*Uchunguzi wa eneo wakati wa kipindi tendaji cha mafunzo ya FMNR © World Vision Ethiopia*

## Vyanzo vya taarifa ya ziada:

- World Vision Australia. (2018). FMNR Manual, Chapter 4: How to practice FMNR. https://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2019/03/FMNR-Field-Manual-Chapter-4_FA.pdf
- World Vision and GIZ. (2021). Forestmaker – Training on FMNR. (Video, 09:46). https://youtu.be/K7aOkCs1PuE?feature=shared

## Hatua na maagizo ya uwezeshaji

*Jedwali 13: Somo la 3.4 muhtasari*

| Muhtasari | Upeo wa kutumia FMNR |
|---|---|
| **Muda** | Dakika 30 |
| **Malengo ya Somo** | Washiriki<br>❖ wanajua aina tofauti za mazingira ambapo FMNR inaweza kutumika<br>❖ wanafahamu azma tofauti ambazo FMNR inaweza kutumiwa |
| **Mada** | ◊ Matumizi ya FMNR katika mazingira tofauti<br>◊ Azma za FMNR |
| **Maandalizi** | • Andaa wasilisho la PowerPoint au chati yenye aina tofauti za mazingira<br>• Andaa wasilisho la PowerPoint au chati kueleza azma tofauti za FMNR |
| **Nyenzo** | o Chati na kalamu<br>o Nyenzo ya video (hiari)<br>o Wasilisho la PowerPoint (hiari) |
| **Mbinu** | ➢ Mawasilisho<br>➢ Majadiliano ya pamoja |

### Hatua na maagizo

**Hatua ya 1:** Watangulize washiriki kwa somo la mwisho la kitengo hiki cha ujifunzaji ambacho kinatangulia kufunga warsha. Eleza kwamba katika somo hili washiriki watajifunza kuhusu aina tofauti za mazingira na azma za matumizi ya FMNR.

**Hatua ya 2:** Eleza mazingira tofauti na mifumo ya matumizi ya ardhi ambayo yanaweza kuelezwa katika sehemu ya usuli wa kiufundi. Unaweza kutumia wasilisho la PowerPoint au chati kutoa maelezo. Ili kuwa na kipindi shirikishi zaidi, rejelelea pendekezo katika 'Maagizo kwa mwendeshaji'.

**Hatua ya 3:** Kisha tanguliza na upitie azma tofauti ambazo zinaweza kunufaika kutokana na matumizi ya FMNR.

**Hatua ya 4:** Baada ya hapo, waalike washiriki na uulize maswali na/au kutoa maoni kuhusu mada zilizowasilishwa katika somo hili.

**Hatua ya 5:** Baada ya kushughulikia maswali na/au maoni, washukuru kwa ushiriki wao tendaji na ufunge kipindi cha mwisho katika kitengo hiki cha ujifunzaji wa FMNR.

### Maagizo kwa mwendeshaji:

Ili kufanya somo hili kuwa shirikishi zaidi kwa washiriki, unaweza kwanza kuwauliza maoni yao kuhusu aina za mazingira ambapo FMNR inaweza kutumiwa kabla ya kuonyesha bango au wasilisho. Mwelekeo sawa unaweza kutumiwa kabla hujaeleza azma yake.

## Kitengo 4 cha ujifunzaji: Kufunga warsha

Hiki ndicho kitengo cha mwisho katika mwongozo huu wa warsha. Kinahitimisha maudhui ya mafunzo na kutoa nafasi ya kushughulikia maswali ambayo bado hayajajibiwa. Washiriki wanakagua malengo yao ya somo na kufanya tathmini binafsi.

*Mchoro 6 Kitengo 4 cha ujifunzaji: Kufunga warsha*

**Somo la 4.1: Hitimisho na tathmini baada ya warsha**

Somo hili linajumuisha hitimisho la warsha kuhusu muhtasari mfupi kuhusu masomo na vipengele vikuu. Isitoshe, Washiriki watafanya tathmini binafsi ya baada ya warsha kulingana na fomu ya tathmini iliyorekebishwa (huku maswali mengi yakisalia kuwa sawa na yale ya tathmini ya kabla ya warsha).

# Somo la 4.1: Hitimisho na tathmini baada ya warsha.

*Jedwali 14: Somo la 4.1 muhtasari*

| Muhtasari | Hitimisho na tathmini baada ya warsha. |
|---|---|
| Muda | Dakika 45 |
| Malengo ya Somo | Washiriki<br>❖ wanaweza kueleza maswali yaliyosalia kuhusu mada na dhana zilizoshughulikiwa katika warsha hii.<br>❖ wametafakari mafunzo yao na kujaza fomu ya tathmini ya baada ya warsha. |
| Mada | ◊ Muhtasari mfupi wa masomo na vipengele vikuu<br>◊ Maelezo ya maswali ambayo bado hayajajibiwa.<br>◊ Kutafakari kuhusu malengo ya somo.<br>◊ Tathmini ya kibinafsi<br>◊ Tathmini |
| Maandalizi | • Onyesha mabango yote na nyenzo zilizotumiwa wakati wa warsha kwenye kuta au ngazi za chati<br>• Tundika bango lenye malengo ya somo ya mafunzo ukutani au kwenye ngazi ya chati<br>• Chapisha nakala ya hojaji ya tathmini ya baada ya warsha kwa kila mshiriki (Kiambatisho B)<br>• Andaa vyeti vya washiriki (hiari) |
| Nyenzo | O Chati<br>O Hojaji za tathmini ya baada ya warsha<br>O Kalamu<br>O Vyeti (hiari) |
| Mbinu | ➢ Mawasilisho<br>➢ Tathmini ya kibinafsi |

**Hatua na maagizo ya uwezeshaji**

**Hatua ya 1:** Wakaribishe washiriki kwa somo la mwisho. Watangulize kwa maudhui ya somo hili: kushereheshea masomo na vipengele vikuu, kufuatiwa na ufafanuzi wa maswali ambayo hayajajibiwa, tafakari ya malengo ya somo na tathmini ya kibinafsi baada ya warsha katika maandishi.

**Hatua ya 2:** Toa muhtasari mfupi wa masomo makuu ya mafunzo haya. Soma kwa sauti mada na vipengele muhimu zaidi vilivyowasilishwa kwenye chati katika masomo ya awali.

**Hatua ya 3:** Wulize washiriki iwapo wako na maswali au maoni yoyote. Elezea maswali yoyote ambayo bado hayajajibiwa kuhusu vipengele vingine vya mafunzo.

**Hatua ya 4:** Angazia malengo ya somo katika mafunzo kama ilivyoonyeshwa kwenye bango Soma malengo kwa sauti ili kuwakumbusha washiriki.

**Hatua ya 5:** Waombe washiriki wote wakamilishe tathmini ya baada ya warsha (Kiambatisho B). Sambaza fomu na utoe muda wa kutosha kwa hatua hii (takriban dakika 30)

**Hatua ya 6:** Baada ya kukusanya hojaji, waombe washiriki kutoa mrejesho kuhusu mafunzo kwa usemi. Zingatia maoni ili kujadiliwa na kuzingatiwa katika mafunzo ya baadaye. Washukuru washiriki kwa mrejesho wo.

**Hatua ya 7:** Ikiwa umeandaa vyeti, watuze. Pongeza kila mshiriki kwa kuhudhuria warsha ya FMNR. Ikiwa inapendeza, mnaweza kupiga picha ya pamoja na kikundi chote.

**Hatua ya 8:** Kabla ya kufunga, waombe wote washiriki katika zoezi hili la mwisho. Zoezi hili litachukua dakika moja tu. Waalike washiriki kujipanga katika mduara. Mduara ukiundwa, waombe wageuke upande wa kulia. Kila mtu aweke mkono wake kwenye bega la kulia la mtu aliye mbele yake. Kila mtu apigepige kwa wepesi bega la mtu aliye mbele yake na kusema, 'Umefanya kazi nzuri'.

**Maagizo kwa mwendeshaji:**

- Usijadili mrejesho wa washiriki (k.m. kueleza kwa nini ulifanya mambo fulani au kwa kujitetea).
- Unapaswa kuweka muktadha kwa vielelezo vilivyotolewa katika Kiambatisho B.
- Inapendekezwa kupitia hojaji na washiriki kabla waanze kuijaza, ili kuhakikisha kwamba kila mtu ameelewa zoezi hili.

# MAREJELEO


Campbell, J. (2002). 'A Critical Appraisal of Participatory Methods in Development Research'. International Journal of Social Research Methodology, 5(1), 19–29. https://www.researchgate.net/publication/248988611.

Center for International Forestry Research. (2017). 'Smallholders and forest landscape restoration in upland northern Thailand'. International Forestry Review, Vol.19(S4), 102–119.

Fedele, G., Donatti, C., Bornacelly, I., & Hole, D.G. (2021). 'Nature dependent people: Mapping human direct use of nature for basic needs across the tropics'. Global Environmental Change, 71, 1–9. https://www.sciencedirect.com/science/article/pii/S0959378021001473

Fischer, G., Wittich, S., & Fründt, S. (2019). Gender analysis in farming systems and action research: A training Manual. International Institute of Tropical Agriculture. https://cgspace.cgiar.org/handle/10568/100149

Food Agriculture Organization (FAO). (2000). On Definitions of Forest and Forest Change. Forest Resources Assessment Programme. https://www.fao.org/3/ad665e/ad665e00.htm#TopOfPage

Garrett, L., Lévite, H., Besacier, C., Alekseeva, N., & Duchelle, M. (2022). The key role of forest and landscape restoration in climate action. FAO. https://doi.org/10.4060/cc2510en

The Global Environmental Facility (GEF). (n.d.). 'Land Degradation'. https://www.thegef.org/what-we-do/topics/land-degradation.

Hall, R., Brent, Z., Franco, J., Isaacs, M., & Shergo, T. (n.d.): A Toolkit for Participatory Action Research. https://www.tni.org/files/publication-downloads/a_toolkit_for_participatory_action_research.pdf

Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC). (2018). Global Warming of 1.5°C. An IPCC Special Report on the impacts of global warming of 1.5°C above pre-industrial levels and related global greenhouse gas emission pathways, in the context of strengthening the global response to the threat of climate change, sustainable development, and efforts to eradicate poverty [Masson-Delmotte, V., P. Zhai, H.-O. Pörtner, D. Roberts, J. Skea, P.R. Shukla, A. Pirani, W. Moufouma-Okia, C. Péan, R. Pidcock, S. Connors, J.B.R. Matthews, Y. Chen, X. Zhou, M.I. Gomis, E. Lonnoy, T. Maycock, M. Tignor, and T. Waterfield (eds.)]. 616. https://www.ipcc.ch/sr15/

IPCC. (2022). 'Land Degradation'. Climate Change and Land: IPCC Special Report on Climate Change, Desertification, Land Degradation, Sustainable Land Management, Food Security, and Greenhouse Gas Fluxes in Terrestrial Ecosystems. 345–436. https://doi.org/10.1017/9781009157988.006.

International Union for Conservation of Nature (IUCN). (2015). Land Degradation and Climate Change. The multiple benefits of sustainable land management in the drylands. Issues Brief. https://www.iucn.org/sites/default/files/2022-07/land_degradation_issues_brief_cop21_031215.pdf.

IUCN. (n.d.). 'Forest Landscape Restoration'. https://www.iucn.org/our-work/topic/forests/forest-landscape-restoration.

Muller, A., Lindell, C., de Villier, I., Garrett, J., Ondere, L.., Zoueini, R., Kelly, R., McKenzie, S., Banu Immanuel, S., Jabeen, S., & Yamada Morovic, Y. (2023). Regreening Communities Handbook. World Vision International. https://www.wvi.org/publications/field-guide/climate-change/project-model-handbook-regreening-communities.

United Nations Convention to Combat Desertification (UNCCD ). (2021). Desertification and land degradation and their impact on natural ecosystems and food security. https://unfccc.int/documents/278550

United Nations Environment Programme (UNEP). (n.d.). 'About forests'. https://www.unep.org/explore-topics/forests/about-forests


World Vision Australia. (2018). FMNR Manual. https://fmnrhub.com.au/wp-content/uploads/2019/03/FMNR-Field-Manual_DIGITAL_FA.pdf

World Vision International. (2020). FMNR Definition and key messages.

World Vision International. (2023). Regreening Communities Project Model. https://www.wvi.org/publications/report/climate-change/regreening-communities-project-model

# NYONGEZA

Nyongeza ya 1. Muundo wa kuchora michoro ya uhusiano




Social – Kijamii
Economi- Kiuchumi
Environmental – Kimazin-gira
Technical – Kiufundi
FOCUS - SHABAHA

Kutoka: Fischer at al., 2019.

**Nyongeza ya 2. Aina za uharibifu wa ardhi**

| Aina za uharibifu wa ardhi | Ujelezi |
|---|---|
| **Mmomonyoko wa udongo** | Uharibifu wa ardhi unaweza kutokea kutokana na mmomonyoko unaosababishwa na maji au upepo. Huenda ikahusisha uharibifu wa kibayolojia, |
| **Uharibifu wa udongo kikemikali (upungufu wa virutubisho)** | Hutokea wakati virutubisho mbalimbali katika udongo vinaweza kupotea kupitia upoteaji wa madini na mashapo yaliyomomonyoka |
| **Uharibifu wa muundo wa udongo** | Hutokea kutokana na kuziba, kubana, upungufu wa hewa na kupungua kwaupenyezaji wa udongo. |
| **Uharibifu wa uoto** | Hujumuisha mkusanyiko wa michakato ambayo huenda ikawa ya asili, hasa mabadiliko yatabianchi, ambayo inaweza kusababisha upotevu wa spishi fulani na makazi, kupunguza majani kutokana na upungufu wa upatikanaji wa unyevu au uingiliaji wa spishi vamizi |
| **Ukataji miti** | Ubadilishaji wa maeneo yenye misitu kuwa matumizi yasiyo ya misitu kama vile ardhi yakilimo, upanuzi wa miji, maeneo yaliyokatwa miti au ardhi ya nyika yanaweza kusababisha uharibifu wa ardhi. Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), ukataji miti ni ubadilishaji wa misitu kwa matumizi mengine ya ardhi au upunguzaji wa miti kwa muda mrefu kufikia kiwango cha chini ya asilimia 10%. |
| **Uharibifu wa misitu** | Mchakato unaosababisha upunguaji wa wingi au maumbile ya uoto na vijenzi vya spishi unaotokea kwa muda au kwa kudumu. Ni mabadiliko ya sifa za msitu ambayo yanasababisha kupungua kwa uwezo wa uzalishaji kutokana na ongezeko la machafuko. |
| **Uharibifu wa rasilimali ya maji** | Michakato mbalimbali ya uharibifu wa rasilimali ya maji inajumuisha mabadiliko katika wingi, ubora wa maji pamoja na mabadiliko katika ruwaza za mtiririko wamaji katika mito. Hutokana na uharibifu wa rasilimali za maji ya juu na chini ya ardhi pamoja na mabadiliko ya ruwaza za mtiririko wa maji katika mito, uharibifu wa ubora wa rasilimali za maji na uwezo wa kuhifadhi na uchafuzi wa maji |

Chanzo: Kwa mujibu wa FAO, 2000, na UNCCD, 2021.

## Nyongeza ya 3. Kanuni elekezi za urejeshaji wa misitu na mazingira

| Kanuni elekezi | Ujelezi |
|---|---|
| **Kuzingatia mandhari** | Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) hutukia katika na baina ya mandhari yote, bali sio maeneo maalum, huwakilisha taswira za mwingiliano wa matumizi ya ardhi na desturi ya usimamizi chini ya mifumo mbalimbali ya umiliki na utawala. Ni katika ngazi hii ambapo vipaumbele vya kiikolojia, kijamii na kiuchumi vinaweza kusawazishwa. |
| **Dumisha na uimarishe mifumo asili ya ikolojia katika mandhari** | Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) au uharibifu wa misitu asili au mifumo tofauti ya ikolojia. Inahimiza uhifadhi, ufufuaji, na usimamizi endelevu wa misitu na mifumo mingine ya ikolojia. |
| **Husisha washikadau na usaidie utawala shirikishi** | Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) huwahusisha washikadau katika ngazi tofauti, ikiwemo vikundi vilivyo hatarini, katika kupanga na kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi, urejesho wa malengo na mikakati, mbinu ya utekelezaji, ushiriki wa manufaa, na mchakato wa tathmini na ukaguzi. |
| **Janibisha kwa muktadha uliopo kwa kutumia mielekeo mbalimbali** | Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) unapaswa kurekebishwa kuafiki mahitaji ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi na maadili ya kiikolojia, na historia ya mandhari. Inatumia sayansi ya kisasa na mbinu bora pamoja na maarifa ya kimapokeo na ya kiasili, na kutumia taarifa hiyo katika muktadha wa uwezo wa ndani na miundo iliyopo au mipya ya utawala. |
| **Rejesha uamilifu anuwai kwa manufaa mengi** | Uingiliaji wa Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) unalenga kurejesha uamilifu mbalimbali wa kiikolojia, kijamii na kiuchumi katika mandhari tofauti na kuzalisha mazao na huduma mbalimbali za mfumo wa ikolojia yenye manufaa kwa washikadau mbalimbali. |
| **Simamia ifaavyo kwa ustahimilivu wa muda mrefu** | Urejesho wa misitu na mandhari (FLR) unalenga kuimarisha ustahimilivu wa mandhari na washikadau wake kwa muda wa kipindi cha kati na kipindi kirefu. Mielekeo ya urejesho inapaswa kuimarisha spishi na uanuwai wa kinasaba na kurekebishwa kadri ya wakati ili kuakisi mabadiliko ya tabianchi na hali nyingine za kimazingira, ufahamu, uwezo, mahitaji ya washikadau na maadili ya kijamii. Kadri urejeshaji unavyoendelea, taarifa kutoka kwa shughuli za ufuatiliaji, utafiti na mwongozo wa washikadau unapaswa kujumuishwa katika mipango ya usimamizi. |


Kutoka: IUCN (n.d.).

## Nyongeza ya 4. Manufaa ya FMNR

| Manufaa ya kiuchumi | Manufaa ya kijamii | Manufaa ya kimazingira |
|---|---|---|
| • Ongezeko la mazao (maradufu au mara tatu zaidi)<br>• Ongezeko la chakula cha wanyama kutokana na majani yanayolika, magamba ya mbegu, na ardhi ya malisho kwa mifugo.<br>• Tija ya juu ya mifugo na uwezo wa kuendelea kuishi.<br>• Kupungua kwa athari kutokana na mafuriko na ukame - miti inapotoa mapato mbadala na vyanzo vya riziki, athari zinapungua na urejeshaji unafanyika haraka.<br>• Kuongeza mapato kupitia mseto na uimarishaji wa shughuli, kama vile kuuza bidhaa za miti.<br>• Athari za mtiririko wa kiuchumi kama vile ajira na uwezo mkubwa wa ununuzi.<br>• Ongezeko la shughuli za kiuchumi huibua fursa kama vile uundaji wa miundo mipya ya biashara ikijumuisha vyama vya ushirika na vikundi vya kuweka akiba. | • Ongezeko la mazao (mara nyingi maradufu au mara tatu zaidi).<br>• Ongezeko la chakula cha wanyama kutokana na majani yanayolika, magamba ya mbegu, na ardhi ya malisho kwa mifugo.<br>• Ongezeko la usalama wa chakula na lishe (kujumuisha<br>• matunda, kokwa na mbegu).<br>• Umbali mdogo kwa wanawake na watoto kusafiri kutafuta kuni.<br>• Kuimarisha uwezo wa jamii kunaweza kusaidia watu kukabiliana na serikali za mitaa, za kikanda na kitaifa pamoja na wadhibiti.<br>• Kuboresha utawala kupitia ufafanuzi wa sheria na kanuni za umiliki wa miti.<br>• Elimu na mafunzo ya kilimo na uuzaji.<br>• Kupungua kwa haja ya vijana na wanaume kuhamia mijini.<br>• Mapato ya juu huzalisha fursa bora zaidi kama vile matibabu, elimu ya watoto, lishe na mavazi.<br>• Uwezeshaji wa wanajamii kuishi kwa kujitegemea na kuwa na matumaini ya siku zijazo. | • Ongezeko la mazao (mara nyingi maradufu au mara tatu zaidi).<br>• Ongezeko la chakula cha wanyama kutokana na majani yanayolika, magamba ya mbegu, na ardhi ya malisho kwa mifugo.<br>• Kupungua kwa mmomonyoko wa udongo<br>• Kupungua kwa uvukizi wa unyevu wa udongo kutokana na vizuia upepo, kivuli na matandazo.<br>• Kuongezeka kwa rutuba ya udongo kupitia viumbe hai kutoka kwa miti.<br>• Kuboresha muundo wa udongo kupitia ongezeko kubwa la rutuba.<br>• Kuongezeka kwa uingizaji wa maji na urejeshaji wa maji ya chini ya ardhi.<br>• Kuongezeka kwa unauwai wa mimea na viumbe, urejeshaji wa mazingira na wingi wa miti.<br>• Kuimarika kwa ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. |

Kutoka: World Vision Australia, 2018.

**Nyongeza ya 5. Gurudumu la maswali kwa FMNR**




| |
|---|
| What is FMNR? - FMNR ni nini?<br>Who Implements FMNR? - Nani anatekeleza FMNR?<br>Why is FMNR important for Livelihoods? – Kwa nini FMNR ni muhimu kwa riziki?<br>When should FMNR be implemented – FMNR inapaswa kutekelezwa lini?<br>How should FMNR be IMpelemented – FMNR inapaswa kutekelezwa vipi? |

Chanzo: Imetolewa kwenye Fischer at al., 2019.

# KIAMBATISHO

**Kiambatisho A. dhana ya warsha ya FMNR Maudhui na ratiba (siku moja)**

Imeandaliwa kwa ushirikiano baina ya World Vision Germany, World Vision Kenya na World Vision Ethiopia kupitia mradi uliofadhiliwa na BMZ, 'Mradi wa Upanuzi wa FMNR nchini Ethiopia na Kenya'.

| Muda | Kitengo/Somo | Maudhui ya somo | Muundo wa somo | Matokeo ya somo | Nyenzo za mafunzo |
|---|---|---|---|---|---|
| **08:30 – 09:00** | | Usajili wa washiriki | | Washiriki wamesajiliwa. | Fomu ya usajili wa washiriki (ya karatasi au ya kidijitali) |
| **Kitengo 1 cha ujifunzaji: Ufunguzi wa warsha** | | | | | |
| **09:00–09:15** | 1.1 Makaribisho na utangulizi | Waendeshaji wa warsha wanawakaribisha washiriki, kujieleza na kueleza sababu ya jumla ya kuwa na warsha hii (ikiwa warsha inafanyika kama sehemu ya mradi, usuli wa mradi unaelezwa kwa muhtasari) Baadaye, kwa kutegemea muktadha wa kitamaduni na ukubwa wa kikundi, kila mshiriki anaweza kupewa nafasi ya kujitambulisha kwa kifupi (jina, nyumbani, jamii. n.k.) | Wasilisho na majadiliano ya pamoja | ▸ Washiriki wanajua shabaha kuu ya maudhui ya warsha hii<br>▸ Washiriki na waendeshaji wa warsha wanapata kufahamiana | Chati imeandaliwa ikiwa na ukurasa wa makaribisho |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **09:15–09:20** | 1.2 Kanuni na sheria za ufunzaji za warsha hii | Somo hili linatanguliza baadhi ya kanuni za ufunzaji na sheria za warsha hii (zimejikita katika kanuni za ufunzaji wa watu wazima): ujifunzaji wa pamoja na wa uzoefu, tafakari na mahusiano. | Wasilisho na majadiliano ya pamoja | ▸ Washiriki wanafahamu kanuni za kimsingi za ufunzaji katika warsha hii<br>▸ Washiriki wanajua sheria za kimsingi za mienendo wakati wa warsha hii. | Chati yenye kanuni na sheria kuu (ambayo inaweza kutundikwa kwenye ukuta wa chumba cha mafunzo)) |
| **09:20–09:30** | 1.3 Maudhui ya warsha na malengo ya somo | Maudhui ya warsha na malengo ya somo yanatangulizwa. Somo hili pia linapaswa kujumuisha chaguzi za washiriki kueleza matarajio yao na malengo ya somo | Mawasilisho na majadiliano ya pamoja (kukiwa na chaguo la washiriki kueleza malengo yao ya somo, ambayo yanaandikwa kwenye chati | ▸ Washiriki wanafahamu upeo na maudhui ya warsha hii)<br>▸ Washiriki wameeleza malengo na matarajio yao ya somo (ikiwa inahusika)<br>▸ Washiriki na waendeshaji wawarsha wamekubaliana kuhusu malengo ya somo ya warsha. | Chati yenye muhtasari wa upeo na maudhui ya warsha Chati yenye muhtasari wa malengo ya somo ya washiriki |
| **09:30–09.45** | 1.4 Tathmini ya kabla ya warsha | Ili kutathmini malengo ya somo ya warsha, washiriki watajaza fomu ya tathmini ya kibinafsi na baada ya mafunzo yenye maswali yanayohusu maudhui ya warsha na masomo. Kwa washiriki wasiojua kusoma na kuandika, hii pia inaweza kufanywa kwa kusaidiwa na mwezeshaji wa warsha. | Fomu/hojaji ya tathmini (hii inapaswa kuwa fupi na inayolenga vipengele muhimu vya mafunzo) | ▸ Washiriki wametathmini ufahamu wao na uwezo kuhusu FMNR kabla ya warsha | Fomu za tathmini ya kabla ya warsha, kalamu |
| **Chai ya asubuhi (09:45–10:00)** | | | | | |
| **Kitengo 2 cha ujifunzaji: Uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili** | | | | | |
| **10:00–11:15** | 2.1 Michoro ya uhusiano ya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili | Katika somo hili, washiriki watatafakari vijenzi na vipengele vya uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili katika miktadha ya maisha yao binafsi.<br>Hii itafanyika kupitia kwa uchoraji wa mchoro wa uhusiano ambao unaruhusu kupata ruwaza ya vijenzi na vipengele pamoja na uhusiano wake.<br>Mchoro wa uhusiano utadhihirisha jinsi washiriki wanachukulia uharibifu wa kimazingira na ukataji miti katika nyumba na jumuiya zao, vipengele ambavyo wanahusisha na dhana hizi mbili, na jinsi wanavyozielewa. | Michoro ya uhusiano | ▸ Washiriki wametafakari na kutambua vipengele muhimu vya uharibifu wa kimazingira katika muktadha wao binafsi<br>▸ Washiriki wametafakari kuhusu na kutambua vipengele na vichocheo vya ukataji miti katika familia na jamii yao<br>▸ Washiriki wametafakari kuhusu na kutambua mikakati na mbinu za sasa za usimamizi wa mali asili katika familia na jamii yao | Chati (moja kwa kikundi cha washiriki 4 hadi 6), kalamu za rangi tofauti |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **11:15–11:45** | Masuala ya msingi kuhusu uharibifu wa mazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili | Somo hili linatoa utangulizi mfupi wa dhana hizi tatu na mahusiano yake makuu.<br>Kila inapowezekana, wawezeshaji wa warsha watafanya viungo kwa matokeo kutokana na michoro ya uhusiano | Wasilisho na majadiliano ya pamoja | ‣ Washiriki wanafahamu vipengele na dhana muhimu za uharibifu wa kimazingira, ukataji miti na usimamizi wa mali asili.<br>‣ Washiriki wanafahamu viungo muhimu baina ya dhana hizi tatu<br>‣ Washiriki wanafahamu athari kuu za uharibifu wa kimazingira na ukataji wa miti kwa riziki | Chati zenye karatasi na kalamu |
| **11:45 –12:15** | 2.3 Utangulizi kwa urejesho wa misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii ) | Katika kitengo hiki, washiriki wanatangulizwa kwa kifupi kwenye dhana ya urejesho wa misitu na mandhari (FLR) iliyo katika jamii Lengo ni kwamba washiriki waelewe ulinzi wa miti na uoto kama suluhu inayowezekana kumaliza ukataji wa miti na uharibifu wa ardhi. Ili kutimiza azma hii, wawezeshaji wa warsha watawasilisha manufaa ya kimsingi kwa mazingira ya miti na uoto kwa hewa katika sehemu maalum, muundo na ubora wa udongo., na usimamizi wa maji. | | ‣ Washiriki wako na uelewa wa kimsingi wa dhana ya urejesho wa mandhari na misitu unaojikita katika jamii<br>‣ Washiriki wanafahamu athari chanyaza kimazingira za miti na uoto mwingine kwa hewa katika sehemu maalum, muundo na ubora wa udongo., na mifumo ya maji. | |
| **Chamcha (12:15-13:00)** | | | | | |
| **Kitengo 3 cha ujifunzaji: Ukuaji Upya wa Miti na Mimea kwa Usimamizi wa Mkulima (FMNR)** | | | | | |
| **13:00–14:00** | 3.1 Utangulizi kwa FMNR | Katika somo hili, tutatanguliza dhana ya FMNR kupitia kwa "gurudumu la maswali", kwa kujadili 'Nini? Kwa nini? Nani? Wapi? Na Vipi? Kipindi hiki kitawaruhusu washiriki kutafakari na kujadili kila mojawapo ya maswali haya matano, huku wawezeshaji wa warsha wakichangia vipengele muhimu kwa kila swali. Hii pia itajumuisha wasilisho la manufaa makubwa ya riziki ambazo FMNR inaweza kusaidia. | Muundo: Gurudumu la maswali (mtindo shirikishi) | ‣ Washiriki wameelewa kwamba FMNR inalenga ukarabati wa uoto uliopo tayari.<br>‣ Washiriki wanaelewa tofauti na uhusiano uliopo baina ya FMNR na upandaji wa miti.<br>‣ Washiriki wanafahamu kwamba FMNR inajumuisha mbinu ya kiufundi na mchakato wa maendeleo ya jamii<br>‣ Washiriki wanafahamu manufaa ya kimazingira na uwezo wa kujikimu unaosaidiwa na FMNR<br>‣ Washiriki wanafahamu kwamba FMNR ni kitendo endelevu ambacho kinahitaji msaada wa jamii nzima. | Chati zenye karatasi, kalamu, Nyenzo ya video (hiari) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ▸ Washiriki wameelewa kwamba FMNR inahitaji kuunganishwa na hatua nyingine za kujikimu na mbinu za usimamizi wa mali asili. | |
| **14:00–14:15** | 3.2 FMNR kama mbinu ya kiufundi | Somo hili litaangazia vipengele vya mbinu ya FMNR (chagua, pogoa, simamia, tumia) | Wasilisho na majadiliano ya pamoja | ▸ Washiriki wanajua vijenzi vinne vya mbinu ya FMNR<br>▸ Washiriki wako na uelewa mzuri wa kinadharia kuhusu utendaji wa kila mbinu | Chati zenye karatasi, kalamu, Nyenzo ya video (hiari) |
| **14:15–14:45** | 3.3 FMNR kama mchakato wa maendeleo ya jamii | Vipengele vya mchakato wa FMNR (unganisha, panga, wezesha) vinatangulizwa kwa lengo la kuwaelewesha washiriki kwamba FMNR inahitaji uanzishaji wa mipangilio fulani ya jamii na taasisi/kanuni (k.m., matumizi ya miti na rasilimali nyingine za asili). | Wasilisho na majadiliano ya pamoja | ▸ Washiriki wanajua vijenzi vikuu vya mchakato wa FMNR<br>▸ Washiriki wanafahamu miundo muhimuna taasisi zinazohitajika kuanzisha FMNR katika jamii (k.m., kamati za usimamizi wa mali asili, sheria ndogo, mipango ya matumizi ya ardhi, n.k.) | Chati zenye karatasi, kalamu, Nyenzo ya video (hiari) |
| **14:45–15:15** | 3.4 Upeo wa kutumia FMNR | Somo hili linatanguliza aina tofauti za mandhari na azma ambapo FMNR inaweza kutumiwa (k.m., shamba, ardhi ya malisho, misitu). | katika Wasilisho na majadiliano ya pamoja (kukiwa na uchunguzi kifani/mifano) | ▸ Washiriki wanajua aina tofauti za mazingira ambapo FMNR inaweza kutumika<br>▸ Washiriki wanafahamu azma tofauti ambazo FMNR inaweza kutumiwa | Chati zenye karatasi, kalamu, Nyenzo ya video (hiari) |
| **Chai ya adhuhuri (15:15-15:30)** | | | | | |
| **Kitengo 4 cha ujifunzaji: Kufunga warsha** | | | | | |
| **15:30– 16:15** | 4.1 Hitimisho na tathmini baada ya warsha . | Somo hili linajumuisha hitimisho la warsha kupitia muhtasari mfupi wa masomo na vipengele vikuu. Washiriki pia watafanya tathmini binafsi ya baada ya warsha kulingana na fomu ya tathmini iliyorekebishwa (huku maswali mengi yakisalia kuwa sawa na yale ya tathmini ya kabla ya warsha). | Wasilisho na fomu ya tathmini ya baada ya warsha | ▸ Washiriki waliweza kueleza maswali yaliyosalia kuhusu mada na dhana zilizoshughulikiwa katika warsha hii.<br>▸ Washiriki wametafakari kuhusu mafunzo yao na kujaza fomu ya tathmini ya baada ya warsha. | Fomu za tathmini ya baada ya warsha, kalamu |
| **16:15** | Mwisho wa warsha | | | | |

## Kiambatisho B. Tathmini ya kabla na baada ya warsha

Tathmini ya ufahamu, kujitolea na uwezo wa washikadau kuhusu FMNR

Tarehe: ______________________________

Eneo: ______________________________

Hujambo mshiriki wa mafunzo,

Asante kwa kukubali kushiriki katika tathmini hii. Tathmini hii ni sehemu ya mafunzo ya FMNR ambayo unahudhuria au ambayo umehudhuria. Tunakuomba utumie muda wako kujaza hojaji hii (sehemu tano) Tafadhali jibu maswali yaliyo hapa chini kulingana na maagizo kwa kila sehemu inayohusika na – iwapo ungependa – toa taarifa za ziada katika maandishi. Tathmini hii itarudiwa katika muda wote wa mafunzo kwa ajili ya kulinganisha na kutusaidia kutathmini athari ya mafunzo. Asante kwa maoni na ushirikiano wako!

*Maelezo ya Faragha ya Data: Utaoji wa taarifa katika hojaji hii ni wa hiari.*

### Sehemu ya 1: Ufahamu wa FMNR

**Maagizo:** Tafadhali weka alama (X) kuonyesha ni kwa kiwango gani kila kauli inahusika kwako.

| # | 1 = chini sana<br>5 = juu sana<br>N.A. = haihusiki/siwezi kujibu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | N/A |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Je unawezaje kukadiria... | | | | | | |
| 1) | Kiwango cha maarifa yako ya jumla kuhusu FMNR? (Je, umesikia kuhusu FMNR hapo awali?) | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 2) | Ufahamu wako wa manufaa ya FMNR? (Je, unajua kuhusu athari chanya za FMNR?) | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 3) | Ufahamu/uelewa wako wa msambao wa sasa (upeo wa matumizi) wa FMNR katika nchi yako? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 4) | Ufahamu/uelewa wako wa uwezo wa sasa (upeo wa matumizi) wa FMNR katika nchi yako? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |

## Sehemu ya 2: Ufahamu wa FMNR

**Maagizo:** Tafadhali weka alama (X) kuonyesha ni kwa kiwango gani kila kauli inahusika kwako.

| # | 1 = chini sana<br>5 = juu sana<br>N.A. = haihusiki/siwezi kujibu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | N/A |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Je unawezaje kukadiria... | | | | | | |
| 1) | Kiwango cha Maarifa yako ya jumla kuhusu FMNR? (FMNR ni nini?) | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 2) | Ufahamu wako kuhusu mielekeo mitatu ya FMNR (mbinu za kiufundi, mchakato wa maendeleo ya jamii, mabadiliko ya mawazo)? ) | | | | | | |
| | Comment: | | | | | | |
| 3) | Ufahamu wako kuhusu uhusiano baina ya FMNR na upanda-ji wa miti? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 4) | Ufahamu wako kuhusu jinsi FMNR inaweza kufungamanishwa na usimamizi wa mali asili na/au shughuli za kuchuma riziki? | | | | | | |
| | Maelezo | | | | | | |

**Maagizo:** Tafadhali weka alama ya (X) hapa chini kwenye jibu moja pekee kwa kila swali (kuna jibu moja tu ambalo ni wazi na sahihi kwa kila swali).

1) FMNR inasimamia nini?
- ❒ Farm Managed Natural Restoration
- ❒ Farming for Maintaining Natural Resources
- ❒ Farmer Managed Natural Regeneration
- ❒ Family Managed Nutritional Recovery

2) Je, unaweza kueleza vipi ufahamu wako kuhusu uhusiano baina ya FMNR na upandaji wa miti?
- ❒ FMNR na upandaji wa miti ni dhana mbili kinzani na haziwezi kuunganishwa
- ❒ FMNR ni sawa na upandaji wa miti
- ❒ Upandaji wa miti unaweza kuwa kipengele jalizi kwa FMNR
- ❒ Upandaji wa miti ni hatua ya kwanza ya FMNR

3) Je, hatua kuu za kutekeleza FMNR ni zipi??
- ❒ Chagua spishi na visiki au miti, pogoa na usimamie, tunza na utumie
- ❒ Chagua na uzalishe spishi za miche, panda na usimamie, tunza na utumie
- ❒ Chagua na ununue spishi za miche, panda na usimamie, tunza na utumie
- ❒ Chagua spishi na miti, ikate miti, ipande upya katika mazingira faafu zaidi, tunza na utumie

4) Je, FMNR ni faafu kwa urejesho wa mazingira ya aina gani?
- ❒ Misitu na mashamba
- ❒ Ardhi ya misitu
- ❒ Misitu na ardhi ya malisho
- ❒ Aina zote zilizopo hapo juu

5) FMNR ni nafuu zaidi kuliko upandaji wa miti?
- ❒ Ni kweli
- ❒ Si kweli

6) FMNR si mwelekeo unaojitegemea na unahitaji kufungamanishwa na hatua nyingine za usimamizi wa mali asili na/au uchumaji riziki.
- ❒ Ni kweli
- ❒ Si kweli

## Sehemu ya 3: Uwezo kuhusu FMNR

**Maagizo:** Tafadhali weka alama (X) kuonyesha ni kwa kiwango gani kila kauli inahusika kwako.

| # | 1 = chini sana<br>5 = juu sana<br>N.A. = haihusiki/siwezi kujibu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | N/A |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Je unawezaje kukadiria... | | | | | | |
| 1) | Uwezo wako wa kueleza FMNR? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 2) | Uwezo wako wa kujumuisha/kutumia/kuendeleza FMNR katika kazi yako ya kila siku? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 3) | Uwezo wako wa kutanguliza/kuendeleza FMNR katika shirika lako/mahali pa kazi? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 4) | Mahitaji yako ya uwezeshwaji zaidi kuhusu FMNR? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 5) | Uwezo wako wa kufanya maonyesho tendaji ya FMNR? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |

**Maagizo:** Tafadhali onyesha hapa chini ni kwa kiwango gani kila kauli inahusika kwako.

1) Je, umewahi kushiriki katika kipindi cha mafunzo kuhusu utendaji wa FMNR?

❒ Ndiyo
❒ La

i. Iwapo ndiyo, vipindi vingapi?

❒ 1
❒ 2-5
❒ Zaidi ya 5

2) Je, umewahi kuendesha kipindi tendaji cha mafunzo kuhusu FMNR?

❒ Ndiyo
❒ La

i. Iwapo ndiyo, vipindi vingapi?

❒ 1
❒ 2-5
❒ Zaidi ya 5

ii. Ikiwa ndiyo, ilikuwa kwa vikundi gani vya washikadau?

❒ Wafanyakazi wa serikali
❒ Washiriki watekelezaji
❒ Mkulima mahiri
❒ Mkulima limbukeni
❒ Nyingine (tafadhali eleza hapa chini)

______________________________

3) Je, umewahi kuzuru eneo la maonyesho ya FMNR?

❒ Ndiyo
❒ La

## Sehemu ya 4: Kujitolea kwa FMNR

**Maagizo:** Tafadhali weka alama (X) kuonyesha ni kwa kiwango gani kila kauli inahusika kwako.

| # | 1 = chini sana<br>5 = juu sana<br>N.A. = haihusiki/siwezi kujibu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | N/A |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Je unawezaje kukadiria... | | | | | | |
| 1) | Motisha/utayari wako kutumia/kuendeleza/kujumuisha FMNR katika kazi yako ya kila siku? | | | | | | |
| | Maelezo (tafadhali bainisha aina ya shughuli--k.m., uundaji wa sera, majadiliano ya mikakati, utoaji mafunzo, uanahabari, matukio faafu, n.k. | | | | | | |
| 2) | Uwezekano kwamba utatumia/kuendeleza/kujumuisha FMNR katika kazi yako ya kila siku katika siku sijazo? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |
| 3) | Vizuizi kwa kutumia/kuendeleza/kujumuisha FMNR katika kazi yako ya kila siku? | | | | | | |
| | Maelezo: | | | | | | |

## Taarifa ya ziada kusaidia mafunzo haya (hiari)

| # | Swali |
|---|---|
| 1) | Je, ni washikadau gani mahususi ungependekeza wahusishwe katika mafunzo haya? |
| | Maelezo: |
| 2) | Je, una mapendekezo gani kwa mafunzo haya? |
| | Maelezo: |


## Taarifa ya ziada kusaidia mafunzo haya (hiari)

Asante sana kwa kushiriki katika tathmini hii!

Iwapo una maswali kuhusu tathmini au mradi, tafadhali wasiliana na katika nchi yako, ilivyobainishwa hapa chini.s

| Nchi |
|---|
| Jina:<br>Cheo:<br>Shirika/Ofisi:<br>Simu:<br>Barua pepe:<br>Skype |
| Jina:<br>Cheo:<br>Shirika/Ofisi:<br>Simu:<br>Barua pepe:<br>Skype |

Implemented by:




**World Vision Deutschland e. V.**
Am Zollstock 2-4 • 61381 Friedrichsdorf
phone: +49 6172 763-0
info@worldvision.de

**Ofisi ya Berlin**
Luisentraße 41 • 10117 Berlin

worldvision.de